# Nipashe

Jumamosi Julai 10, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580637

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US


**Serikali** kurejesha leseni za maduka ya kubadili fedha

UKURASA 3



**Nyumba** za polisi zilizotelekezwa kuanza kutumika

UKURASA 3




UKURASA 11

# 'Tusisubiri maiti ziokotwe mitaani'

UK. 2




Mitungi ya Oxygen ikishushwa katika Hospitali ya Rufani ya Kanda Bugando, jijini Mwanza jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**.

# Treni ya umeme kuanza Desemba

UKURASA 5




# Mbowe apoteza kaka kwa corona

UKURASA 2


**MICHEZO** SIMBA, YANGA 'MOTO' KUWAKA UK.24

**MAONI, KATUNI** UK.6

# Bugando yapewa mitungi 300

**Na Richard Makore, MWANZA**

SERIKALI imeipa Hospitali ya Rufani ya Kanda Bugando mitungi 300 ya gesi ya Oksijeni kwa ajili ya kuhudumia wagonjwa wenye matatizo ya upumuaji wakiwamo wagonjwa wa corona.

Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Hospitali hiyo, Dk. Fabian Massaga, alithibitisha jana kupokea mitungi hiyo alipozungumza na Nipashe ofisini kwake jijini hapa jana.


Dk. Massaga alisema mitungi hiyo ilikabidhiwa jana asubuhi hospitalini huko na Bohari Kuu ya Dawa (MSD).

Alisema itasaidia kupunguza ukubwa wa tatizo la uhaba wa mitungi ya kuhifadhi gesi ya Oksijeni walilonalo.

Mapema wiki hii, baada ya kumalizika kwa kikao cha wadau wa kupambana na ugonjwa wa corona kilichoongozwa na Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Robert Gabriel, Dk. Massaga alisema walikuwa na mitungi 100 ya kuhifadhi gesi hiyo kwa siku huku mahitaji yakiwa mitungi 300.

Kutokana na uhaba huo, Dk. Massaga aliwaomba wadau kutoa msaada ili angalau ipatikane mitungi 500 kwa siku itakayotosheleza mahitaji ya wagonjwa katika hospitali hiyo.

"Idadi ya wagonjwa wanaofika hospitalini wanaohitaji mitungi ya Oksijeni ni kubwa na hospitali yetu haina mitungi ya kuzalisha kiasi cha kutosheleza, hivyo tunaomba wadau wajitokeze kusaidia ili tuweze kuwahudumia wagonjwa kwa kuwa wagonjwa ni wengi," alisema.



Rais Samia Suluhu Hassan, akizungumza na Naibu Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Mazingira la Umoja wa Mataifa (UNEP), Joyce Msuya, Ikulu jijini Dodoma jana. **PICHA: IKULU**

# 'Tusisubiri maiti ziokotwe mitaani'

**Na Waandishi Wetu**

WAZIRI wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Dorothy Gwajima, amesema ugonjwa wa corona unaendelea kusambaa kwa kasi nchini, akiwataka wananchi kuchukua tahadhari badala ya kusubiri waone nchi inafikia hatua mbaya ya kuokota maiti mitaani.

Amesema licha ya ugonjwa huo kudhibitiwa, wagonjwa wameendelea kujitokeza na kulazwa hospitalini.

Dk. Gwajima aliyasema hayo jana katika Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI) jijini Dar es Salaam na kuwataka wananchi waelewe na wasingojee hali ya kuzoa maiti mtaani ndipo waanze kuchukua tahadhari.

"Kazi inayofanyika ni kufanya hali isiwe mbaya, serikali inajitahidi na Mheshimiwa Rais (Samia Suluhu Hassan) amekuwa akikumbusha 'jamani ndugu zangu tuchukue tahadhari', ili hali hii tunayodhani ipo hivi kwa sababu inashikiliwa kwa juhudi mbalimbali za kinga isije ikapitiliza," alisema.

Waziri huyo alisisitiza kuwa wagonjwa wa corona wapo na wanaendelea kujitokeza na hiyo inamaanisha kwamba maambukizi yapo na siyo ya uongo.

"Ni nguvu kubwa sana inafanyika na watumishi wetu walio mstari wa mbele kuhakikisha hicho watu wanachokisubiri kitokee katika ngazi ile, kisitokee.

"Tunapotoa elimu tunamaanisha kurahisisha mapambano kwa ushirikiano na nchi kwa kuchukua tahadhari," alisema.

Waziri Gwajima alisema licha ya kutoa elimu hiyo, baadhi ya wananchi wanaitikia na wengine hawafanyi hivyo na kuwataka wafanye hivyo ili serikali iongeze wigo ili nchi iwe salama.

"Kwenye msongamano wapo wanaovaa barakoa na wengine hawavai, lakini wewe uliyepona, huumwi, umebeba kimelea na unakisambaza, waokoe basi wengine.

"Kuna wazee, wapo wanaoumwa magonjwa mbalimbali, tunawaokoaje? Wengi tukivaa barakoa, tutaokoa wengine," alisema.

Gwajima alisema kuwa katika kueneza elimu, wanawatumia waganga wa mikoa na halmashauri na wakuu wa wilaya na mikoa husika.

"Tuna tiba asili ambazo hatujazitupa, zilisaidia wengi awali na sasa zinasaidia wengi, watu watumie, wale vyakula ambavyo ni vya asili ili kuongeza kinga.

"Idadi ya wagonjwa kwa sasa siwezi kueleza kwa sababu inabadilika, wanaweza wakawa mia (100) na wakashuka wakawa 50 au wamepanda mpaka 80, kwa hiyo siwezi kusema kwa sasa kwa sababu sijaichukua, lakini itoshe kusema wagonjwa wapo," alisema.

**MITUNGI YA GESI**

Katika hatua nyingine, wizara hiyo imesema inatarajia kuweka mitambo 25 kwenye hospitali zote za mikoa na kanda nchini ili kukidhi uhitaji wa gesi tiba endapo kutakuwa na ongezeko la wagonjwa.

Mkurugenzi wa Kinga wa Wizara hiyo, Dk. Leonard Subi, akizungumza na Nipashe jana kuhusu namna wanavyokabiliana na uhaba wa mitungi ya Oksijeni, alisema wanaendelea na jitihada za kuongeza uzalishaji nchini.

Alisema tayari wamesimika mitambo saba katika hospitali saba nchini zenye uwezo wa kuzalisha mitungi 200 kila moja kwa siku.

Alisema mitambo hiyo yote inaweza kuzalisha mitungi 1,400 kwa siku ikiwa ni nyongeza ya uwezo uliokuwapo awali.

"Hivyo tumeendelea kuboresha mifumo ya mtiririko wa hewa tiba ya Oksijeni kwenye baadhi ya hospitali kwa kujenga mifumo hiyo ili gesi tiba inapozalishwa ipelekwe moja kwa moja kwa mgonjwa," alisema.

Aliwataka wananchi kuchukua hatua zote za kinga na kuzingatia miongozo yote iliyotolewa na wizara ili kuepuka kupata ugonjwa huo.

"Kwa kuzingatia ipasavyo tutakata mnyororo wa uambukizo wa ugonjwa huo, hivyo kujinusuru kuingia kwenye matumizi ya gesi tiba ya Oksijeni," alisisitiza Dk. Subi.

●**Imeandikwa na Romana Mallya na Mary Geofrey**


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P. 2888,
40470 DODOMA, Tovuti:
www.mwtc.go.tz

03 - 07 - 20 21

**TANGAZO**

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya Jumamosi tarehe **10 – 07 – 2021** kampuni ya **Mainline Carriers Ltd.** itasafirisha Mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka **Dar-Es-Salaam** kuelekea **Rufiji**, gari hizo zenye namba za usajili:

   **T 899 DSD / T 416 AYO**
   **T 985 DTN / T 390 DHQ**
   **T 641 DFA / T 387 DHQ**
   **T 918 DSD / T 969 CPS**
   **T 680 DUB / T 974 CPS**
   **T 685 DUB / T 310 DDH**

2. Gari hizo zina vipimo vifuatavyo:

| | | |
|---|---|---|
| Urefu | - | mita 22 |
| Upana | - | mita 4.4 |
| Kimo | - | mita 4.8 |

3. Njia itakayotumika: **Dar es Salaam Port kupitia Mkuranga kuelekea Rufiji**, gari litasafiri muda wa mchana tu (**Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)**

216352402

**Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.**


# Mbowe apoteza kaka kwa corona

**Na Mwandishi Wetu**

MWENYEKITI wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Freeman Mbowe, ametangaza kufiwa na kaka yake, Charles Mbowe, akiweka wazi kuwa chanzo cha kifo hicho kilichotokea juzi katika Hospitali ya KCMC ni maradhi ya corona.

Mbowe alitangaza msiba huo juzi, akibainisha kuwa amelazimika kukatisha ziara yake visiwani Zanzibar kutokana na msiba huo.

"Ndugu Watanzania wenzangu, familia yetu imepatwa na msiba wa kaka yetu Charles Aikaeli Mbowe, ambaye amefariki kwa ugonjwa wa Covid-19 usiku wa kuamkia leo katika Hospitali ya KCMC.

"Kutokana na ukweli kwamba kuna maambukizi mengi ya ugonjwa wa corona, tunaomba Watanzania na waombolezaji walioonyesha kushiriki nasi wachukue tahadhari zote za kujikinga na Covid-19.

"Kwa hiyo, tunaomba mazishi na msiba wote huu tuendeshe kwa utaratibu wa kitofauti, kuna watu wachache sana wa karibu ndiyo watashiriki moja kwa moja katika utaratibu wa kumlaza ndugu yetu Charles," alisema.

Rais Samia Suluhu Hassan alikuwa miongoni mwa watu waliotoa salamu za rambirambi kwa Mbowe kutokana na msiba huo muda mfupi baada ya kiongozi huyo wa CHADEMA kutangaza msiba huo.

"Nakupa pole ndugu Freeman Mbowe na wafiwa wote kwa kuondokewa na ndugu yenu mpendwa Charles Mbowe.

"Nawaombea moyo wa subira, uvumilivu na ustahimilivu katika kipindi hiki cha majonzi. Bwana ametoa na Bwana ametwaa, jina lake lihimidiwe, amina," aliandika Rais Samia kwenye ukurasa wake rasmi wa mtandao wa kijamii wa Twitter.

Katibu Mkuu wa CHADEMA, John Mnyika, katika ukurasa wake wa Twitter, aliandika: "Nimepokea kwa masikitiko taarifa ya kifo cha Charles Mbowe, kaka yake na mwenyekiti. Poleni sana familia ya kaka Charles na ukoo wote wa Mbowe."

Kwa mujibu wa taarifa ya Mbowe, mazishi yanatarajiwa kufanyika Jumatatu Julai 12, mwaka huu kijijini Machame mkoani Kilimanjaro.

HABARI KITAIFA

# Makazi ya polisi yaliyotelekezwa kuanza kutumika

**Na Romana Mallya**

HATIMAYE askari polisi na maofisa wa jeshi hilo wameruhusiwa kuyatumia majengo ya nyumba za makazi yaliyoko Kunduchi na Oysterbay mkoani Dar es Salaam baada ya majengo hayo kukosa wakazi kwa miaka mingi.

Licha ya kukamilika kwa miradi ya ujenzi wa nyumba hizo miaka mitatu iliyopita, askari na maofisa wa Jeshi la Polisi walishindwa kuingia kutokana na mabadiliko ya kisera.

Agizo la kuingia kwenye nyumba hizo lilitolewa jana mkoani Dar es Salaam na Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, George Simbachawene.

Kiongozi huyo aliagiza kuanzia sasa mradi huo wa nyumba za makazi ya askari polisi na maofisa ambao ujenzi wake ulianza mwaka 2014 na kukamilika mwaka 2018, ukiwa chini ya mkandarasi Kampuni ya Mara World Tanzania Limited, uanze kutumika.

"Makazi ya Kunduchi ni kwa ajili ya askari polisi 330 na Mikocheni ni kwa ajili ya maofisa 23," Simbachawene alifafanua.

Mei 22 mwaka huu, waziri huyo, akizungumza na Nipashe, alisema nyumba hizo hazitumiki kutokana na mabadiliko ya kisera yaliyofanyika.

"Kulikuwa na mkataba kati ya serikali na kampuni iliyojenga nyumba hizi ambao baadaye sera zikabadilika, ikawa kwamba maeneo ya jeshi yasiingie mikataba na sekta binafsi," alisema.

Simbachawene alisema kuwa baada ya kubadilika kwa sera, serikali ililazimika kuingia kwenye majadiliano kwa sababu tayari mwekezaji alishawekeza kwenye nyumba hizo.

Juni 7, mwaka huu, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama ilifanya ziara katika mradi huo ambao pia unahusisha ujenzi wa Kituo kipya cha Polisi Oysterbay na kuridhika nao na kupendekeza askari wahamie huku mambo mengine ya mkataba yakiendelea kufanyiwa kazi.

Juni 19, 2019, aliyekuwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Hamad Masauni, alizuru kwenye nyumba hizo na kutoa mwezi mmoja kwa Shirika la Rasilimali la Jeshi la Polisi kutoa vielelezo kwa Kamati ya Tathmini iliyoundwa kwa ajili ya mradi wa Ofisi ya Polisi Oysterbay na nyumba hizo ili zikabidhiwe serikalini.

Juni 5, mwaka 2016, kupitia taarifa ya vyombo vya habari iliyotolewa na wizara hiyo ilieleza kuwa, Katibu Mkuu wake wakati huo, Meja Jenerali Projest Rwegasira, Jeshi la Polisi liliagizwa kuwasilisha mkataba wa miradi hiyo baada ya kubainika ni mikubwa na ya muda mrefu.

Miradi hiyo ilitekelezwa kwa gharama ya Dola milioni 296 baina ya mwekezaji na serikali.



Waziri wa Mambo ya Ndani, George Simbachawene (kushoto), akipokea zawadi kutoka kwa Balozi wa Uturuki nchini, Dk. Mehmet Gulluoglu, baada ya kumaliza mazungumzo yao kuhusu masuala mbalimbali ya ushirikiano katika ulinzi na usalama kati ya nchi hizo mbili, jijini Dar es Salaam, jana. **PICHA: WMNN**

# Serikali kurejesha leseni maduka ya kubadili fedha

**Na Romana Mallya**

WAZIRI wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, ameagiza wataalamu wa wizara hiyo kufanya tathmini ya maduka ya kubadilisha fedha na kurejesha leseni kwa wenye vigezo ambao awali walifutiwa.

Katika mahojiano na Kituo cha Azam TV jana, Dk. Nchemba alisema kwa sasa wanafanya tathmini mpya.

"Tathmini kwa upande wa upatikanaji wa huduma hiyo kupitia benki ilishakamilika. Hatua inayofuata ni tathmini kwenye maduka binafsi ambayo na yenyewe yanaendelea kuratibiwa kadri ya vigezo vilivyowekwa na siku siyo nyingi mtaanza kuona yale yanayokidhi vigezo yataanza kutoa huduma," alibainisha.

Alisema ameshakutana na kufanya mazungumzo na baadhi yao na amezipokea hoja zao na mojawapo walimwambia kuwa hiyo ni kazi yao, hivyo warudishiwe leseni.

"Tayari nimeshawaelekeza watu wangu wafanye tathmini ili wazirudishe, wakirudishwa kazini tutakusanya kodi, kwa hiyo hii ndiyo nimewaambia," alisema.

Waziri Mwigulu alisema hoja ya pili waliyoisema ni kuhusu mtaji uliowekwa umekuwa juu na ameielekeza timu yake ya wataalamu ifanye tathmini. "Kitu ambacho ninataka kuwaomba Watanzania tuelewane vile vitu vinavyokuwa vya kisera ambavyo vina manufaa mapana ya nchi, ni vyema tukajifunza kukubaliana nayo kwa sababu pia tukiwa na nchi ikawa na utakatishaji wa fedha wa kiwango kikubwa au inayotumia fedha ya nchi nyingine inapunguza heshima ya uhuru wetu," alisema.

**VIGEZO**

Alisema vigezo vitakuwapo kwa sababu awali kulikuwa na makosa kwenye uanzishaji wake katika baadhi ya maeneo.

"Hata vituo vya mafuta huwa inashauriwa umbali fulani hivi kama vinafuatana na kama vinatazamana, hata maduka yanatakiwa yampe urahisi yule mtumiaji kwa eneo.

"Ilenge shughuli zinazohitaji zaidi dola na fedha nyingine za kigeni kwa sababu maduka ya fedha za kigeni yasipothibitiwa, ni chanzo kimojawapo cha utakatishaji wa fedha," alisema.

Mbunge wa Arusha Mjini, Mrisho Gambo (CCM) aliliibua suala hilo wakati wa Bunge la Bajeti lililohitimishwa siku 10 zilizopita jijini Dodoma.

Gambo alikosoa uamuzi wa serikali kutumia nguvu kubwa wakati wa kuyafunga maduka hayo, akidai wafanyabiashara wengi walipokwa fedha zao na serikali.

Hata hivyo, Waziri Nchemba alipoulizwa kuhusu hoja hiyo wakati wa mahojiano jana, alisema ni suala la uchunguzi.

"Hakuna eneo ambalo jambo limefanyika bila hatua za kiuchunguzi, hatua za kiuchunguzi huwa zinaleta majawabu tofauti tofauti, kujibu kwa ujumla kwake linaweza lisiwe jibu sahihi kwa maana hiyo lile ni jambo mahususi ambalo kama kuna eneo ambako kulikuwa na taratibu za kiwango hicho linatakiwa kuwa 'treated' kwa umahususi wake.

"Lakini, kwenye hoja ya jumla ni kwamba kulikuwapo na matatizo ya kisera, sehemu nyingine maduka yetu unakuta yamepangana yenyewe eneo moja.

"Sehemu nyingine unakuta fedha iliyopo kwenye maduka ni kubwa kuliko fedha iliyoko kwenye benki, madhara yake ni kushusha thamani ya fedha ya Tanzania, mnakuwa na nchi inayotumia fedha ya nchi nyingine," alifafanua.

Waziri Nchemba alisema ukiwa na maduka ya kubadilishia fedha kila baada ya nyumba moja na fedha zilizopo humo ni nyingi kuliko zilipo benki, hiyo inamaanisha nchi inatumia fedha za kigeni.

SIMBA CEMENT
STRENGTH WITHIN

**INVITATION FOR TENDERS FOR SERVICES**

1. Tanga Cement Public Limited Company Limited is hereby soliciting bids from interested eligible companies and individuals to supply materials and render services listed in the schedule below for the year 2021
2. Interested eligible bidders may obtain a complete set of bidding documents from the office of the Procurement Manager located at the Tanga Cement premises in Tanga between 08H00 and 14H00 on Mondays through Fridays (excluding public holidays).
3. Sealed bids must be deposited in the Tender Box located at the Tanga Cement visitors' gate in Tanga by 12H00 on the 23 July 2021
4. Sealed tenders and modifications thereof must be deposited in the Tender Box located at the visitors' gate by 12H00 on the closing date indicated above. All tenders submitted must be valid for **as specified in tender documents** from the closing date indicated above. All tenders must be sealed, marked with the **relevant tender title** and addressed to:

   **The Managing Director**
   Tanga Cement Public Limited Company
   P O Box 5053
   Tanga – Tanzania
5. This is a mere invitation to bids; it does not constitute an offer to a contract or bind the Company in any way.
6. Tanga Cement is not bound to accept the lowest or any other bid.
7. All bidders must have approved local content from Mining Commission

| S/No. | Tender Tittle |
|---|---|
| 1 | Supply of Printing and photocopying services |
| 2 | Tender for management of labour/manpower |

21635202

# Makala akerwa mazingira mnada wa ng'ombe Pugu

**Na Maulid Mmbaga**

MKUU wa Mkoa wa Dar es Salaam, Amos Makala, ameelezea kutoridhishwa na miundombinu ya mnada wa ng'ombe Pugu na kumwagiza mkandarasi kufanya marekebisho.

Alitoa maagizo hayo jana alipofanya ziara ya kushtukiza katika mnada huo baada ya kupata taarifa za malalamiko ya wananchi kuitaka serikali iingilie kati uboreshaji wa eneo hilo.

Pia Makala alionyesha kutoridhishwa na tabia ya watendaji kutengeneza urasimu na kuchelewesha uboreshaji wa mnada huo ikiwamo ujenzi wa uzio, sakafu, eneo salama la kupakilia ng'ombe, vyoo na kero ya ukosefu wa maji.

"Mazingira niliyoyaona eneo hili na huo urasimu uliopo hautoi matumaini. Kama mtaendelea na mambo yenu ya tathmini, njooni 'site' (eneo la kazi). kazi zinazotakiwa kufanywa zifanywe, za kufanyia tathmini ziendelee lakini kazi iendelee muwapo eneo la kazi.

"Hivi ni vitu vidogo wakati mnaendelea na tathmini ya kujenga ukuta anzeni kurekebisha na vitu vingine. Ng'ombe hapa usalama wake haupo, yaani jinsi palivyo ni sawa na mnada wowote wa kijijini. Sijaridhishwa hata kidogo, naomba lifanyiwe kazi," alisema Makala.

Aliongeza kuwa mambo madogo ya urasimu yanayofanywa na watendaji hao ndiyo yanayojenga imani mbaya kwa wananchi kuwa viongozi wa serikali hawaendi na kasi inayotakiwa katika kushuhulika na kero za wananchi.

Pia aliagiza kuondolewa mara moja matofali yaliyokusanywa katika eneo hilo kwa ajili ya kutumika katika ujenzi wa ukuta unaozunguka mnada huo baada ya kubaini kuwa hayana ubora.



Waziri wa Madini, Dotto Biteko (katikati), akizungumza na Katibu Mkuu wa Shirikisho laVyama vya Wachimbaji Madini Tanzania (FEMATA), Lister Balegele (kushoto), alipotembelea Maonyesho ya 45 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam katika Uwanja wa Mwalimu Nyerere, Barabara ya Kilwa jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Katibu Mkuu CCM atema cheche

**Na Mwandishi Wetu**

WAJUMBE wa Sekretarieti ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) Taifa, wameonya kwamba wao si viongozi wa kupiga porojo na hawako tayari kuona ilani ikihujumiwa.

Katika taarifa yao ya kuhitimisha ziara ya siku mbili mkoani Rukwa, wajumbe hao wakiongozwa na Katibu Mkuu wa CCM, Daniel Chongolo, wamesema katika kusimamia utekelezaji wa ilani ya CCM ya 2020-2021, hawatamvumilia kiongozi au mtendaji serikalini atakayekuwa kikwazo katika kuitekeleza kwa ufanisi.

Wajumbe wengine ni Kanali mstaafu Ngemela Lubinga, ambaye ni Katibu wa Halmashauri Kuu ya CCM Taifa (NEC) Siasa na Uhusiano wa Kimataifa, Shaka Hamdu Shaka, Katibu wa NEC Itikadi na Uenezi na Katibu Mkuu wa Umoja wa Vijana wa CCM (UVCCM), Kenani Kihongosi.

Katika kikao kilichofanyika kwenye ukumbi wa Halmashauri ya Manispaa ya Sumbawanga, mkoani humo juzi, Chongolo alisema, ziara yao iliyoanza Julai 7 hadi 8 kutembelea mashina ya CCM, wameshuhudia miradi ambayo thamani ya fedha hailingani na viwango husika.

Chongolo alitoa mfano kwamba hospitali za wilaya za Nkasi na Kalambo, kila moja imepatiwa Sh. bilioni 2.3, lakini ujenzi hauridhishi kwa sababu thamini ya fedha hailingani na kazi iliyofanyika.

Kutokana na hali hiyo ya ovyo, Katibu Mkuu Chongolo alimwagiza Mkuu wa Mkoa wa Rukwa, Joseph Mkirikiti, kuhakikisha ndani ya siku zisizozidi 14 ujenzi wa hospitali hizo unalingana na thamani ya fedha na kwamba maelekezo hayo si porojo.

"Tunamaanisha, si kurembarembа, ni lazima tufanye kazi yenye tija," alisema Chongolo katika kikao hicho kilichohudhuriwa na viongozi na watendaji wa CCM, viongozi na watendaji wa serikali, madiwani pamoja na wabunge.

"Wananchi wakiona mambo hayaendi, watatuona sisi tunapiga porojo na sisi hatuko tayari kuitwa wapiga porojo," alionya.

Kero nyingine ambayo wananchi wanakumbana nayo ni ukosefu wa dawa katika hospitali, vituo vya afya na zahanati, licha ya serikali kutoa fedha nyingi kuwezesha wananchi kupata huduma hiyo.

Katibu Mkuu atawasiliana na Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, Dk. Doroth Gwajima, pamoja na uongozi wa Bohari Kuu ya Dawa (MSD), kujua mamilioni ya fedha yanayotolewa kwa ajili ya kuwezesha upatikanaji wa dawa yanakwama wapi.

"Tunataka watueleze nani anasababisha mkwamo katika upatikanaji wa dawa. Nasema hivi, sisi viongozi tunawajibu wa kufuatilia na kusimamia thamani ya fedha katika kila eneo," alisema.

Chongolo alisema kila kiongozi na mtendaji katika chama na serikali anawajibu wa kutimiza wajibu wake kwa kuhakikisha upatikanaji wa tija unakuwapo.

Kuhusu migogoro ya ardhi, Chongolo alimwagiza Mkirikiti pamoja na wakuu wa wilaya za mkoa wa Rukwa kutafuta suluhisho la kero hiyo, ambayo imekuwa ikipoteza muda mwingi wa wananchi, ambao wangeutumia katika uzalishaji mali.

Kwa upande wa maji alisema bado ni changamoto, na kudokeza kwamba ni wakati muafaka kuanza kufikiria kuwa na mradi mkubwa wa maji kutoka Ziwa Tanganyika kwa ajili ya Mkoa wa Rukwa.

# Askofu Shoo mwenyekiti mpya CCT

**Na Christina Haule,**
MOROGORO

MKUU wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Askofu Dk. Frederick Shoo, amechaguliwa kuwa Mwenyekiti mpya wa Jumuiya ya Kikristo Tanzania.

Dk. Shoo ambaye pia ni Mkuu wa Dayosisi ya Kaskazini, ataongoza jumuiya hiyo kwa kipindi cha miaka minne ijayo.

Kabla ya uchaguzi huo, Dk.Shoo alikuwa makamu mwenyekiti wa kwanza wa CCT. Makamu mwenyekiti wa pili alikuwa Askofu Dk. Jacob Chimeledya wa Kanisa la Anglikana Dayosisi ya Mpwapwa na Askofu Mkuu mstaafu wa kanisa hilo.

Katika uchaguzi uliofanyika mjini Morogoro sambamba na Mkutano Mkuu wa 31 wa CCT, Dk. Shoo alishinda kinyang'anyiro hicho baada ya kupata kura 63 kati ya 212 zilizopigwa.

Wengine walioingia katika kinyang'anyiro hicho na kura zao kwenye mabano ni Askofu Dk. Stanley Hotay wa Kanisa la Anglikana Dayosisi ya Mount Kilimanjaro (50) na Askofu Mkuu wa Kanisa la Moravian Tanzania, Dk. Alinikisa Cheyo, aliyekuwa anatetea nafasi hiyo (47).

Askofu Mkuu wa Kanisa la Anglikana Tanzania na Askofu wa Dayosisi ya Tanga, Dk. Mahimbo Mndolwa alipata kura 29 na Askofu Mkuu wa Kanisa la Africa Inland Church Tanzania (AICT) na Askofu wa Dayosisi ya Geita, Mussa Magwesela (23).

CCT ni taasisi ya kikristo inayounganisha makanisa 12 na vyama 12 nchini vikiwamo vya kitaifa na kimataifa.

Makanisa hayo ni KKKT, AICT, Moravian, Anglikana, Kanisa la Baptist Tanzania, Jeshi la Wokovu Tanzania, kanisa la Presbyterian Afrika Mashariki, Kanisa la Biblia, Kanisa la Mungu Tanzania, Kanisa la Kiinjili Tanzania (ECT) na Kanisa la Upendo wa Kristo Masihi (KIUMA).

Vyama wanachama ni Chama cha Biblia Tanzania, Chama cha Vijana Wanaume Tanzania (YMCA), Chama cha Vijana Wanawake Tanzania (YWCA), East Africn Enterprise (EAE), Life Ministry na Emmanuel International.

Vingine ni Summer Institute of Linguistics, Compassion International Tanzania, Dodoma Christian Medical Centre, Mission Aviation Fellowship (MAF) na Scripture Un-

HABARI KITAIFA

# Treni ya SGR Dar- Moro rasmi Desemba



Na Mwandishi Wetu

TRENI ya umeme itakayotumia reli ya kisasa (SGR) kutoka Dar es Salaam hadi Morogoro, inatarajia kuanza kutoa huduma Desemba, mwaka huu.

Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mhandisi Dk. Leonard Chamuriho (pichani juu), alisema hayo jana alipokuwa akizindua Bodi mpya ya Wakurugenzi wa Shirika la Reli Tanzania (TRC) jijini Dar es salaam.

Kutokana na hali hiyo, Waziri Chamuriho aliitaka bodi hiyo kwa kushirikiana na menejimenti ya TRC kuhakikisha maandalizi yote ya msingi ya kuwezesha kuanza kwa usafiri huo yanakamilika ifikapo Novemba.

"Hakikisheni treni ya kisasa itakayotumia reli ya SGR sehemu ya Dar es Salaam hadi Morogoro inaanza ili kuwawezesha wananchi kunufaika na fursa hiyo mpya kiuchumi," alisema.

Dk. Chamuriho alisema serikali itaendelea kuikarabati reli ya sasa 'meter gauge' na kuongeza vichwa vipya vya treni na mabehewa ili iendelee kutoa huduma katika ubora unaotakiwa wakati ujenzi wa reli ya kisasa SGR ukiendelea.

"TRC ni lazima muwe na maarifa ya kibiashara ili hatua ya serikali kukarabati na kununua mabehewa mapya iendane na kasi ya kusafirisha shehena nyingi na mizigo mizito kwa reli, hivyo kupunguza mzigo mzito katika barabara", alisisitiza.

Pia aligusia umuhimu wa bodi na menejimenti ya TRC kuhakikisha maboresho ya muundo yanaendana na maslahi ya wafanyakazi ili kuongeza morali na kuleta tija katika shirika hilo.

Naye Mwenyekiti wa Bodi ya TRC, Prof. John Kondoro, alisema wamejipanga kuhakikisha shirika linatoa huduma ya kisasa, haraka na kwa gharama nafuu na watahakikisha reli ya sasa inapitika wakati wote wa mwaka.

Mkurugenzi Mkuu wa TRC, Masanja Kadogosa, alisema hadi sasa asilimia 92 ya ujenzi wa SGR kati ya Dar es salaam na Morogoro umekamilika wakati sehemu ya Morogoro- Makutopora hadi Singida umefikia asilimia 65.

Kukamilika kwa reli ya SGR na uboreshaji unaofanywa katika reli yote ya sasa, kutahuisha huduma za usafiri na uchukuzi nchini, hivyo kuchochea uzalishaji na biashara za ndani na nje ya nchi na hivyo kukuza uchumi.

Wakati huo huo, Waziri Chamuriho jna alizindua Bodi ya Chuo cha Bahari (DMI) na kuitaka bodi hiyo kuhakikisha inakisaidia chuo kuongeza idadi ya wataalam wa bahari.

Sambamba na hiyo, alikitaka kuwa na takwimu sahihi za mabaharia nchini na kuisaidia nchi katika azma ya kufufua uchumi wa bluu.

# Kortini tuhuma kukutwa na vipande 17 meno ya tembo

Na Kulwa Mzee

WATU wanne waliokutwa na meno 17 ya tembo maeneo ya Mbande wamefikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu kwa tuhuma za kukutwa na nyara za serikali kinyume cha sheria.

Washtakiwa walifikishwa jana na kusomewa mashtaka mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi Rashid Chaungu.

Akisoma mashtaka hayo, Wakili wa Serikali, Salim Msemo, aliwataja washtakiwa kuwa ni Eliakimu Sanga (52), Mwashani Duma (38), Anitha Muheve (35)na Kumbuka Kimanda (35).

Alidai kuwa washtakiwa kwa pamoja wanadaiwa kutenda kosa hilo Juni 28, mwaka huu, katika eneo la Mbande Magengeni, wilayani Temeke.

Siku hiyo, alidai kuwa washtakiwa walikutwa na nyara za serikali, ambazo ni vipande 17 vya meno ya tembo vyenye thamani ya Dola za Marekani 75,000 sawa na Sh 173, 925, 000 mali ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania bila kuwa na kibali kutoka kwa Mkurugenzi wa Wanyamapori.

Baada ya kusomewa mashtaka, hawakutakiwa kujibu kwa kuwa mahakama hiyo haina mamlaka ya kusikiliza shauri lao hadi ipate kibali kutoka kwa Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP).

Wakili Msemo alidai upelelezi wa kesi hiyo haujakamilika.

Hakimu Chaungu aliahirisha kesi hiyo hadi Julai 22, mwaka huu, itakapotajwa na washtakiwa wamerudishwa rumande.

TRA

MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA

Imethibitishwa na ISO 9001: 2015

TAARIFA KWA UMMA KUHUSU TRA KUKUTANA NA WADAU WA FILAMU NCHINI

Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), itakutana na wadau wa Filamu nchini siku ya **tarehe 10 Julai, 2021** kwa ajili ya kujadili kodi mbalimbali zinazogusa mazao ya filamu ikiwemo Kodi ya Zuio (Withholding Tax) na Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT).

Katika kikao hicho, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) itakuwepo kutoa ufafanuzi juu ya sera ya matangazo ya biashara kwenye chaneli za kulipia (Pay TV).

Aidha, Bodi ya Filamu Tanzania ikiwa ni Taasisi inayosimamia Sekta ya Filamu na Michezo ya Kuigiza nchini itahudhuria kama mlezi wa tasnia hiyo.

Kikao hicho kitafanyika katika ukumbi wa Chuo cha Kodi (ITA) **P.O.Box 9321, Mikocheni Dar es salaam Tel: +255 22 2216800/1** au **+255 783081348 Email: ita@tra.go.tz kuanzia saa 7:00 mchana.**

Wadau wote wa filamu nchini wanakaribishwa.

***"Pamoja Tunajenga Taifa Letu"***

Imetolewa na;
**KAMISHNA WA KODI ZA NDANI**

216349502

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Ratiba Ligi Kuu msimu ujao isiendekeze viporo

**KUMALIZIKA** kwa msimu huu wa Ligi Kuu Tanzania Bara, ni ishara wazi kwamba maandalizi kuelekea katika msimu mpya wa 2021/22 yameshaanza.

Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu wa 2020/21 inatarajiwa kukamilika ifikapo Julai 18, mwaka huu kwa timu zote 18 kushuka kwenye viwanja mbalimbali hapa nchini kucheza mechi za kufunga pazia la ligi hiyo. Ligi hiyo ambayo inasimamiwa na Bodi ya Ligi Nchini (TPLB), iliyoko chini ya Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), ndio hutoa mwakilishi au wawakilishi wa Bara katika mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika na Kombe la Shirikisho.

Msimu huu pia utakamilishwa na mchezo mwingine wa fainali ya mashindano ya Kombe la FA utakaochezwa Julai 25, mwaka huu kwenye Uwanja wa Lake Tanganyika ulioko mkoani Kigoma na ambapo bingwa wake atapata tiketi ya kushiriki michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika moja kwa moja.

Kubakia kwa idadi chache ya mechi za kumaliza msimu na kuelekea kwa fainali ya Kombe la FA, ni dalili tayari wasimamizi wameshaanza maandalizi ya msimu mpya hasa kwa kuzingatia upungufu na changamoto zilizojitokeza katika msimu huu unaoelekea ukingoni. Moja ya changamoto iliyopigiwa kelele na wadau wa soka nchini ni upangaji wa ratiba wa mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara na zile za michuano ya Kombe la FA.

Ratiba yenye viporo vingi imeonekana kuongeza changamoto kwa timu ambazo mara kadhaa zilikutana na 'maumivu' hayo kutokana na michezo yake kuahirishwa na hivyo kuwafanya makocha na wachezaji kuharibu programu zao walizoziandaa kwa ajili ya kushuka uwanjani kuwakabili wenzao.

Tunafahamu kutokana na jiografia ya nchi za kiafrika, mechi za viporo hazikwepeki, lakini TFF hakikisheni viporo hivyo visizidi, kwa sababu vinaleta 'ukakasi' hasa kwa wale ambao vinawagusa na pia vinapunguza ladha kwa mchezo kwa sababu klabu iliyoguswa na janga hilo hujikuta inalazimika kucheza mechi zake mfululizo.

Na kwa kufanya hivyo huatarisha afya za wachezaji lakini pia baadhi yao hushindwa kuonyesha viwango vizuri kwa sababu ya uchovu waliokuwa nao.

Mechi za viporo zinachangia kupunguza 'utamu' wa ligi kwa sababu timu zinazocheza baadaye zinaingia uwanjani tayari zikifahamu matokeo watakayopata yatawaweka kwenye nafasi ipi tofauti na pale klabu zote zinaposhuka dimbani kusaka pointi tatu kwa pamoja.

Kama timu moja tu (Simba), ilipofika hatua ya robo fainali, pamoja na Namungo iliyocheza hatua ya makundi kulikuwa na viporo zaidi ya vinne, je, msimu ujao ambao Tanzania itakuwa na wawakilishi wanne katika mashindano hayo yanayosimamiwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF), tutakuwa na viporo vingapi? TFF isione aibu kwa kuchukua ujuzi kutoka katika nchi zilizoendelea na kuiga mfumo wao wa kupanga ratiba za ligi zao za ndani unavyofanyika na hatimaye mambo yatakwenda vizuri.

Pia suala la kusimamisha Ligi Kuu kwa muda ili kutoa nafasi kwa Timu ya Taifa (Taifa Stars), kujiandaa na michezo ya kimataifa linatakiwa kuandaliwa upya kwa sababu wachezaji wanapokuwa kwenye timu zao na kucheza mechi zenye ushindani, huwa ni bora kuliko kukusanyika pamoja kwenye kambi ya Stars na kufanya mazoezi mepesi huku wakisubiri walioko nje ya nje kuwasili.

Makocha wa timu za taifa, klabu na wadau wa soka huu ni wakati wenu wa kuwasilisha maoni wakati maandalizi ya msimu mpya yakiwa yameshaanza na wahusika wakifungua milango ya kupokea mapendekezo ya kuboresha kanuni zitakazotumika katika msimu mpya ambao tunatarajia uwe bora zaidi na wenye ushindani hasa kutokana na mabilioni ya udhamini yaliyotangazwa kutolewa na wadhamini mbalimbali.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Dunia hadaa ulimwengu shujaa

Na barnabas Maro

**DUNIA** ina madanganyo mengi na shida nyingi, hivyo inahitaji mtu shujaa. Methali hii yatufunza dunia ina shida na madanganyo ya kila aina, kwa hiyo hatuna budi kuwa na werevu wa kuikabili lau (tamko la kuonyesha majuto) sivyo tutaangamia.

"Huu mpira tulioshinda niliucheza siku nne, lakini hii fainali mbona tayari nishaicheza na nimepata nafasi kubwa." Haya ni maneno ya mzee fulani wa Yanga anayetamba kuiwezesha timu hiyo kuifunga Simba na kuifunga mabao mengi zaidi kwenye mchezo wa fainali ya Kombe la FA utakaofanyika Julai 25, mwaka huu mkoani Kigoma.

Alisema bila kificho kuwa: "Simba wajiandae mimi nina watu, sifanyi mimi ila nawaandalia mazingira, wakisema wanataka hiki na hiki nawapa. Mpira tuliocheza na kushinda niliucheza siku nne kabla lakini hii fainali mbona tayari nimeshaucheza na nimepata nafasi kubwa.

Uchawi ni kitu chochote kinachotumiwa na mganga wa kienyeji kuleta madhara kwa mtu mwingine. Ufundi wa kutumia dawa au maandishi maalumu ya uganga ili kuleta madhara kwa viumbe; sihiri, zana zinazotumika kurogea.

"Amelaaniwa mtu yule amtegemeaye mwanadamu, amfanyaye mwanadamu kuwa kinga yake, na moyoni mwake amemwacha Bwana. Maana atakuwa kama fukara nyikani, hatoona yatakapotokea mema. Bali atakuwa jangwani palipo ukame, katika nchi ya chumvi isiyokaliwa na watu. Amebarikiwa mtu yule anayemtegemea Bwana, ambaye Bwana ni tumaini lake." (Yeremia 17:5-7).

"Maana atakuwa kama mti uliopandwa kando ya maji, uenezao mizizi yake karibu na mto; hautoona hofu wakati wa hari ujapo, bali jani lake litakuwa bichi; wala hautahangaika mwaka wa uchache wa mvua, wala hautaacha kuzaa matunda. Moyo huwa mdanganyifu kuliko vitu vyote, una ugonjwa wa kufisha; nani awezaye kuujua?" (Yeremia 17:8-9).

Dua ni maombi yanayoelekezwa kwa Mungu; maombi ya mja kwa Mola wake ili apate mahitaji yake; maombi: omba dua. Sidhani kama kuna dini inayoruhusu urogaji; uchawi na kama ipo, basi ni ya kishetani.

'Uchawi' ni mtu anayewaroga watu, mtu anayewadhuru watu kwa njia ya kishirikiana, yaani tabia ya kuamini mambo ya ramli na uchawi. 'Ushirikina' ni tabia ya kuamini uwezo wa kiumbe kingine juu

> **"Maana atakuwa kama mti uliopandwa kando ya maji, uenezao mizizi yake karibu na mto; hautoona hofu wakati wa hari ujapo, bali jani lake litakuwa bichi; wala hautahangaika mwaka wa uchache wa mvua, wala hautaacha kuzaa matunda. Moyo huwa mdanganyifu kuliko vitu vyote, una ugonjwa wa kufisha; nani awezaye kuujua?" (Yeremia 17:8-9).**

yako badala ya ule wa Mwenyezi Mungu.

Yafaa tujue kuwa 'ulozi' ni tendo la kumpatia mtu shida au hasara kwa uchawi, tendo la kuroga. Utendewaji ubaya wa kumroga mtu.

Timu zetu za kandanda zinasahau kuwa" Baraka ya Mungu humsononesha mtu." Maana yake neema zinazotokana na Mungu humfanya mtu akanyookewa na mambo yake. Hii ni methali inayofunza umuhimu wa kumcha Mungu ambaye ndiye aliyeviumba vyote- mbingu na vyote vilivyo duniani.

Klabu zetu zinapaswa kuacha tabia ya kuthamini uchawi na badala yake kuwekeza nguvu kwenye mazoezi na kufuata maelekezo ya walimu wao. Kadhalika waachane na ulevi wa pombe, matumizi ya dawa za kulevya na mambo ya tamaa kwa kina dada.

Jambo lililonishtua kabla ya mechi iliyopita kati ya Simba na Yanga hivi karibuni ni TFF kutangaza kuwa wachezaji wa timu hizo wangepimwa kama wanatumia dawa za kuwapa nguvu!

Tangazo hilo lilishangaza kama ninavyoshangazwa na vitisho vya Polisi wanapowaonya majambazi kuwa watawafuata kwenye maficho yao kwani watawasaka mpaka wawakamate. Nani atabaki kusubiri akamatwe? Matangazo kama hayo yapaswa kufanywa kwa kushitukiza na si vinginevyo.

Na ili kutekeleza majukumu yake, wahusika wanapaswa kuwafanyia vipimo wachezaji wa timu mbalimbali na si kutegea kusubiri mechi hiyo kubwa wakati Ligi Kuu Tanzania Bara peke yake kwa msimu mmoja ina michezo zaidi ya 300. Zoezi kama hilo linatakiwa pia kufanyika kwa ligi za madaraja ya chini na katika michezo mingine na wahusika wasikae kutolea macho wacheza kandanda peke yake.

Jambo la siri hufanywa kwa siri kwani unapomtangazia mkosaji au mtuhumiwa kuwa utamkagua ni sawa na kumwambia ajiandae kuhojiwa au kukamatwa. Hata wanyama wanapowinda hawangurumi bali hunyatia tu bila kelele ndipo hukamata.

marobarnabas@yahoo.com
0784 334 096



Mkuu wa Wilaya ya Iringa mjini, Mohamed Moyo (katikati), akijadiliana jambo na Askofu wa kanisa la Anglikana Dayosisi ya Ruaha, Joseph Mgomi (kulia), alipomtembelea nyumbani kwake, wilayani humo juzi, kwa ajili ya mazungumzo na kujitambulisha. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Maofisa ununuzi, chanjo kikaangoni

**Na Grace Mwakalinga,** ILEJE

MKUU wa Wilaya ya Ileje, Anna Gidarya, amemwagiza Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Haji Mnasi kuwasimamisha kazi Ofisa Ununuzi, Safina Shapwata na Ofisa Chanjo, Jacob Mwang'unda.

Maofisa hao wanatuhumiwa kufanya ununuzi wa vifaa vyenye kutia shaka vya thamani ya Sh. milioni 90.

Amesema amebaini ukiukwaji mkubwa katika ununuzi na kwamba kamati za ununuzi ngazi za vijiji zilizoundwa zilikuwa hewa kwa kuwa ziliingizwa kwenye mfumo wa malipo na kusababisha kuwapo kwa miyororo ya ulaji wa fedha za miradi ngazi ya kijiji hadi wilaya.

Akizungumzia juzi suala hilo aliahidi kula sahani moja na maofisa hao huku akiwatahadharisha wanaondelea na mchezo mchafu wa kutafuna fedha za serikali. "Namwomba mkaguzi wa ndani kutoa ripoti ya miradi iliyokataliwa na kamati ya siasa ndani ya siku 14 ili kufahamu thamani ya fedha na hali halisi ya miradi iliyojengwa kwa lengo la kuwabaini waliohujumu au kukwamisha miradi hiyo," alisema Gidarya.

Hivi karibu, akiwa katika ziara ya kukagua miradi ya maendeleo, Mkuu wa Mkoa wa Songwe, Omary Mgumba, aliwataka watendaji kuwa waadilifu na kutimiza wajibu wao kwa mujibu wa matakwa ya utumishi wa umma.

Aliwataka watumishi wa umma kwa kushirikiana na wananchi kuongeza uzalishaji wa mazao na kuongeza thamani ili kupata uhakika wa soko la ndani na nje ya nchi hasa kutumia ukanda wa nchi za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC).

# Wakatisha masomo kwa kupewa ujauzito

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

WANAFUNZI 30 wanaosoma katika shule mbalimbali wilayani Shinyanga, wamedaiwa kupewa ujauzito na kukatisha masomo yao kwa kipindi cha miezi sita, huku wengine 12 wakitoroshwa kwenda kuolewa.

Mkuu wa Dawati la Jinsia Wilaya ya Shinyanga kutoka Jeshi la Polisi mkoani Shinyanga, Victoria Maro, alibainisha hayo juzi wakati akizungumza na vyombo vya habari. Alisema hali ya matukio ya ukatili wa kijinsia wilayani humo si ya kuridhisha na kwamba kwa kipindi cha Januari hadi Juni, mwaka huu, wanafunzi 30 wameshapewa ujauzito, 12 wametoroshwa, 44 walibakwa na watoto wa kiume 12 kulawitiwa.

"Tatizo ambalo linasababisha matukio haya ya ukatili wa kijinsia kuendelea hapa Shinyanga ni kufichwa kwa ushahidi ili kulinda watuhumiwa, wazazi wa watoto kushindwa kutoa ushindi na kusababisha watuhumiwa kuachiwa huru na kuendeleza matukio haya kwa wanafunzi na kuzima ndoto zao," alisema Maro.

"Mfano mzuri sasa hivi tuna kesi ya mwanafunzi wa kidato cha tatu aliyekuwa akisoma Shule ya Sekondari Tinde kupewa ujauzito na tukamkamata mtuhumiwa. Lakini cha ajabu mwanafunzi amemkana mwanamume huyo na kumtaja mtu mwingine ambaye ni dereva wa roli ambaye amesema hamjui kitu ambacho ni ngumu kwetu kumtia hatiani," aliongeza.

Mmoja wa wanafunzi ambaye amepewa ujauzito na kuacha masomo mkazi wa kijiji cha Nsalala wilayani Shinyanga (jina limehifadhiwa), alisema alikutana na dereva wa roli na kisha kumrubuni na kwenda kufanya naye ngono wilayani Nzenga mkoani Tabora na kumpa ujauzito, hivyo kuzima ndoto zake za kuwa mwalimu.

Mtendaji wa Kijiji cha Nsalala, William Mnyasi, alisema elimu bado inahitajika kwa wanafunzi hasa ya masuala ya afya ya uzazi, makuzi na wazazi kuwajibika kwa watoto wao ipasavyo hasa wa kike, kwa kuwatimizia mahitaji yao ya shule ili kuwaepusha na vishawishi.

# Madereva wamlilia DC ubovu barabara

**Na Steven William**, IRINGA

MADEREVA wanaobeba abiria katika pikipiki za Bajaji katika mitaa mbalimbali ya Manispaa ya Iringa, wamelalamikia ubovu wa barabara kuwa ni chanzo cha vyombo vyao kuharibika.

Viongozi wa vyama vya madereva wa bodaboda, Bajaji, teksi na daladala katika manispaa ya iringa, walitoa malalamiko hayo juzi katika mkutano wao na Mkuu wa Wilaya ya Iringa, Mohammed Moyo.

Mwenyekiti wa Chama cha Madereva wa Bajaji, Melabu Kihwele, alisema kutokana na ubovu wa barabara za mitaa ya Manispaa ya Iringa, bajaji zinakufa, hivyo vijana kukosa ajira.

Alisema Bajaji hizo madereva wanapewa kwa mkataba na wamiliki lakini zinakufa mapema kutokana na ubovu wa barabara matokeo yake vijana wanakosa ajira na familia zao kubaki kukaa bila kipato.

Katibu wa Umoja wa Madereva wa Daladala Manispaa ya Iringa, Shaibu Maruzuku, alisema kunatokea ugomvi wa mwingiliano wa masilahi kati ya biashara ya bajaji na daladala kwa kuingiliana katika njia za kupita, hatua ambayo ilisababisha serikali kuingilia kati.

Alisema Jeshi la Polisi kupitia Kikosi cha Usalama barabarani na Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Ardhini (LATRA) wamekuwa chanzo cha migogoro katika vyombo vya moto vya usafirishaji abiria kutokana na kuwanyanyasa madereva wa bodaboda, bajaji na daladala.

Katika hatua nyingine, viongozi wa vyama vya wafanyabiashara katika Manispaa ya Iringa wamesema machinga wamekuwa wakisababisha kero katika soko la mashine tatu na soko kuu la Iringa kwa kupanga biashara zao katika barabara za kupita magari.

Mwenyekiti wa wafanyabiashara katika soko la Mashine Tatu, Jafari Sewando, alisema mbele ya Moyo kuwa machinga wamekuwa na tabia ya kupanga biashara katika maeneo ya barabara zinazopita vyombo vya moto jambo ambalo ni hatari kwa maisha yao.

Pia walisema kuna wafanyabiashara wameanzisha ukamuaji mafuta ya alizeti katika viwanda vyao vidogo vidogo lakini tatizo ni umeme kukatika mara kwa mara, hivyo kufanya gharama za kufanya shughuli hiyo kuwa kubwa.

Akijibu kero hizo, Moyo alisema amesikia na atazifanyia kazi na baadaye kuzitolea majibu akiwa na viongozi wa manispaa hiyo kwa kuwaita tena makundi hayo ili wasikie maagizo atakayoyatoa.

# Mkurugenzi aita vijana ajira Sekta ya Kilimo

**Na Waandishi Wetu**

SERIKALI imewataka vijana kuacha kuzurura katika miji mikubwa nchini kwa kisingizio cha kutafuta ajira, badala yake wawekeze kwenye kilimo alichosisitiza kuna uhakika wa ajira na fursa nyingi.

Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI), Dk. Geofrey Mkamilo, alitoa kauli hiyo jana alipozungumza na vijana mbalimbali waliotembelea banda la taasisi hiyo kwenye Maonesho ya 45 ya Biashara ya Kimataifa, maarufu Sabasaba mkoani Dar es Salaam.

Alisema kuna dhana kutoka kwa vijana kukiona kilimo kama sehemu ya mateso wakati siyo lazima ulime, bali unaweza kuwekeza kupitia kilimo hicho kwa kuongeza mnyororo wa thamani au kusindika kwa kupitia mazao yanayozalishwa na wakulima mbalimbali nchini.

"Kuna dhana potofu iliyopo hivi sasa kwa vijana kuwa kilimo hakilipi na ni sehemu ya mateso, hivyo ni bora kutafuta kazi, lakini mimi leo ninawambia kilimo siyo lazima ushike jembe ukalime.

"Unaweza kununua mazao yaliyolimwa na wakulima ukayaongezea thamani kwa kusindika na kuuza ikawa sehemu ya ajira yako na wapo vijana wamepata utajiri kupitia sekta hii. Changamkieni hiyo fursa haraka vijana," alisema. Mkurugenzi huyo alitolea mfano kilimo cha zabibu kinachofanywa katika Mkoa wa Dodoma ambako baadhi ya vijana wananunua mchuzi wa zabibu na kutengeneza mvinyo na kuuza ndani na nje ya nchi na kujipatia fedha kama waajiriwa wengine, huku wengine wakinunua zabibu hizo kwa wakulima na kuuza kwa wastani wa Sh. 5,000 kwa kilo na kuendesha maisha yao kama sehemu ya ajira za kudumu.

Alisema zao lingine ambalo lina fursa nyingi ni pamoja na zao la korosho ambalo lina bidhaa nyingi ikiwamo kuuza korosho yenyewe, kutengeneza mabibo ili kuwa mvinyo na kuuza.

Alisema cha msingi kinachotakiwa kwa vijana ni kuwa na andiko la biashara na kuliwasilisha kwa taasisi za kifedha kama Benki ya CRDB na benki zingine zinazotoa mikopo ya kilimo.

"Sisi kama TARI tuna wataalamu wa kutosha kabisa na hapa tulipo katika maonyesho ya Sabasaba tunaonyesha na fursa mbalimbali kuanzia kulima hadi kuchakata mazao na kusindika katika mnyororo wa thamani.

"Vijana waje kupata elimu hiyo bure tunayotoa ili wawekeze katika kilimo na kuachana na tabia kuzunguka mijini bila kazi yoyote," alisema mkurugenzi huyo.

Mratibu wa Taifa wa Usambazaji wa Teknolojia za Utafiti wa Kilimo kutoka TARI, Mshaghuley Ishika, alisema wanakusudia kuhakikisha teknolojia zote zilizofanyiwa utafiti zinawafikia wakulima na wafanyabiashara wanaotaka kuwekeza katika kilimo cha mazao mbalimbali ili wazalishe kwa tija na kuuza ndani na nje ya nchi.

Mratibu wa Kitaifa wa Uzalishaji na Biashara wa TARI, Kisa Mwaisoba, alisema lengo la teknolojia hizo ni kuwafanya wakulima na wafanyabiashara nchini kuzalisha kibiashara ili kujiongezea kipato kitakachotumika kwenye shughuli zingine za kijamii ikiwamo elimu.

**●Imeandaliwa na Ashton Balaigwa na Ahmad Njama, SJMC**

## Chifu wa Wasukuma kuzikwa leo

**Na Rose Jacob,** MWANZA.

ALIYEKUWA Chifu wa Bukumbi wa Kabila la Wasukuma wilayani Misungwi mkoani Mwanza, Charles Ilago, anatarajiwa kuzikwa leo kijijini kwake.

Akizungumza kwa niaba ya familia, mjukuu wa marehemu, Magreth John, alisema mwili wa Mtemi Ilago unatarajiwa kuzikwa leo.

"Mtemi Ilago alizaliwa mwaka 1928 na alisimikwa kuwa mtemi mwaka 1944 na kufikisha idadi ya watemi 23, amefariki akiwa na miaka 93," alisema Magreth.

Akizungumza kwa niaba ya washauri wa Mtemi (Wanan'ghoma), Mwenyekiti wa Ukoo wa Bakumbi, Aloyce Kipondya, alisema Mtemi Ilago atazikwa katika makaburi ya watemi wa Bukumbi yaliyoko Kigongo Feri.

"Mtemi Ilago ilikuwa anaishi Kijiji cha Idetemya wilayani Misungwi na kwa mujibu wa taratibu za kitemi, anapofariki dunia mtemi, huwa inakuwa siri na watu wanashangaa tu wanaona mtemi mpya," alisema Kipondya.

Kipondya alisema kutokana na hali ya sasa, teknolojia imebadilika ndiyo maana tumepiga ngoma za kuashiria kifo cha mtemi ili wananchi waje msibani.

Gloria Munhambo, Ofisa Msimamizi wa Bodi ya Utalii Tanzania, Ofisi ya Kanda ya Ziwa, alisema wamepokea kwa masikitiko kifo hicho.

Alisema kuwa wao kama taasisi ya serikali, wamepoteza ngao katika kuendeleza mambo ya mila na desturi za Kitanzania.

"Kiukweli Mtemi Ilago alikuwa ni mtu aliyependa kudumisha mila zetu na alikuwa ni mwenye kumpenda Mungu tangu nimemfahamu. Hii kwa kweli imenigusa sana," alisema Munhambo.



Mmoja wa wanafunzi wa shule ya wasichana ya Kikwe ya jijini Arusha, akiwa amekalia moja ya kitanda, baada ya Taasisi ya Vodacom Foundation, kukabidhi vitanda na magodoro 100 kwa shule hiyo jana, ikiwa ni hatua ya kuunga mkono elimu ya mtoto wa kike. Wa tatu kushoto ni Mkuu wa Idara ya Uhusiano na Mawasiliano Vodacom Tanzania, Jacquiline Materu na (kushoto) ni Mkuu wa shule hiyo, Alex Kitomari. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Majaliwa ataka huduma PASS ziwafikie wakulima

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

WAZIRI Mkuu Kassim Majaliwa, ameuomba uongozi wa asasi isiyo ya kiserikali ya PASS Trust kuhakikisha huduma zake zinasambaa nchi nzima ili kuwanufaisha wajasiriamalia wa kilimo.

Akizungumza jijini Dodoma wakati wa uzinduzi wa kampeni ya kitaifa ya upandaji zabibu, Majaliwa alisema PASS Trust imefanya kazi kubwa katika kuchochea upatikanaji wa mikopo kwa ajili ya wakulima nchini.

"Nimetembelea nchi nzima, nimefika Kigoma wakati wa kampeni ya kilimo cha michikichi, nimekwenda Tanga kuhamasisha kampeni ya kilimo cha mkonge na nilikuta wakulima waliosaidiwa na PASS Trust kujiendesha. Mnafanya kazi kubwa PASS Trust," alisifu.

Majaliwa alisema kuna haja asasi hiyo inayosaidia dhamana kwa wakulima kwa asilimia 20 hadi 60, kufungua matawi mengi nchi nzima ili kuwezesha wakulima wengi kunufaika na huduma zao.

Majaliwa aliitaka PASS Trust kuhakikisha inafungua ofisi ya kimkaka mjini Dodoma ili kuwasaidia wakulima wa mkoa huo na mikoa jirani.

"Zabibu sasa ni zao la kimkakati pamoja na mengine manane na tunahitaji ushirikiano wenu kuinua uzalishaji wake," Majaliwa alisema.

Kaimu Mkurugenzi wa PASS Trust, Anna Shanalingigwa, alisema asasi hiyo itafanyia kazi ushauri wa waziri mkuu kuhakikisha huduma zake zinawafikia wajasiriamali wengi katika wa kilimo biashara.

"Mpaka sasa tumewezesha wakulima wa zabibu ndani ya Mkoa wa Dodoma kupata mikopo inayofikia Sh. bilioni mbili katika benki tunazoshirikiana nazo.

"Kiasi cha Sh. bilioni 3.5 kiko mbioni kutolewa kwa udhamini wetu kuwafikia wakulima wa zabibu takriban 400," Shanalingigwa alibainisha.

Alisema wako tayari kuwasaidia wakulima wa zao hilo Dodoma na mikoa mingine kupata kuboresha kilimo hicho.

Naibu Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, alisema wizara iko katika mazungumzo na PASS Trust kutanua fursa za kilimo hicho mkoani Dodoma na nchi nzima.

Kwa sasa PASS Trust ina ofisi kwenda kanda sita, ikiwamo Kanda ya Ziwa waliko na ofisi Mwanza inayosaidia Mwanza, Bukoba, Shinyanga na Simiyu, Kanda ya Magharibi wakiwa na ofisi Kigoma, Tabora na Katavi.

Kanda ya Mashariki wana ofisi Morogoro ikitoa huduma Morogoro, Dodoma, Singida, Dar es Salaam, Pwani na Zanzibar).

Kanda ya Kaskazini wana ofisi Arusha inayotoa huduma Arusha, Kilimanjaro, Manyara na Tanga na Nyanda za Juu Kusini wana ofisi Mbeya inayohudumia mikoa ya Mbeya, Iringa na Songwe.

Kusini wana ofisi Mtwara ikihudumia mikoa ya Mtwara, Lindi na Ruvuma. Asasi hiyo ina ofisi za makao makuu yake mkoani Dar es Salaam.



# Baraza NGO lapata viogozi wapya

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

BARAZA la Taifa la Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (NaCoNGO) limetekeleza maagizo ya serikali baada ya kufanya uchaguzi na kuwapata viongozi watakaoliongoza kwa kipindi cha miaka mitatu.

Juni 7, mwaka huu, Waziri wa Afya Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wazee na Watoto, Dk. Dorothy Gwajima, alifanya uteuzi wa kamati ya mpito kwa ajili ya kuratibu na kusimamia uchaguzi wa baraza hilo.

Kamati hiyo iliundwa na wajumbe 10 kutoka katika mashirika yasiyo ya kiserikali ya kitaifa na kimataifa na ilipewa siku 30, kufanikisha uchaaguzi huo.

Katika uchaguzi huo, Lilian Badi alichaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Baraza, Revocatus Sono kuwa Katibu Mkuu na John Kiteve kuwa Mweka Hazina pamoja na wajumbe wanane wa Kamati na Bodi. Akizungumza juzi mara baada ya kutangaza matokeo, Mwenyekiti wa Kamati ya Uchaguzi, Wakili Fraviana Charles, alisema anaishukuru wizara kupitia ofisi ya msajili kuiteua kamati ya mpito ya kuratibu uchaguzi wa NaCoNGO.

"Kwa niaba yao naomba niseme wamefanya kazi nzuri ambayo ndiyo imetukutanisha hapa na wanastahili pongezi,"alisema Charles.

Aidha, aliwataka viongozi wapya waliochaguliwa kwenda kufanya kazi kwa weledi, kwa moyo wa kujitolea na kwa ushirikiano wa karibu na serikali kwa maslahi ya Watanzania.

Pia alisema kwa waliokosa nafasi, wakubali matokeo na kusonga mbele kwa kushirikiana na viongozi waliochaguliwa ili kuijenga NaCoNGO mpya.

"Nahimiza umoja na mshikamano katika kujenga NaCoNGO mpya kwa manufaa ya sekta na taifa kwa ujumla,"alisema Charles.

Mwenyekiti wa Bodi ya Uratibu wa NGO, Richard Simbaiga, alisema uchaguzi huo umepita, hivyo makundi yote yanatakiwa kuvunjwa kwa maslahi ya baraza hilo.

Vilevile, aliwataka viongozi waliochaguliwa kuwa wasimamizi wa Asasi zote na siyo kubwaa pekee yake.

Alisema takwimu zinaonyesha kuwa kuna usajili wa aidi ya NGO 11,000 nchini lakini ambazo zinaoneka kuwa hai hazizidi 4,000.

"Hivyo viongozi mnayo kazi ya kwenda kuhakikisha hizi NGO zingine 7,000 ambazo hazijulikani ziko wapi, zinafufuliwa na kutoa machango katika kusukuma maendeleo ya taifa letu," alisema Simbaiga

Aliwataka viongozi hao kuhakikisha kuwa wanaimarisha mifumo ya taasisi hizo katika kufanya kazi zao kwa ufanisi ikiwa ni pamoja na kuimarisha mahusiano ndani ya NGO na serikali kwa ujumla.

## Aweso atoa maagizo saba

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WAZIRI wa Maji, Jumaa Aweso, ametoa maagizo saba kwa watumishi wa wizara hiyo, likiwemo la kumsimamisha Ofisa Ugavi wa Bonde la Ziwa Tanganyika, Victor Kaphifa, kwa kosa la kufanya udalali na kuichafua taswira ya wizara.

Maagizo mengine aliyotoa ni wizara hiyo kufuatilia madeni yote ya wizara na taasisi, mamlaka za maji, kukagua madeni na madai yaliyowasilisha, hoja za CAG zipatiwe majibu.

Pia aliagiza kutumia fedha za wizara kwa ajili ya kuendeleza miradi ya maji pamoja na kwenda kufanya kazi kwa ushirikiano ili kuinua sekta ya maji, kushirikiana na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) kuleta mfumo wa ununuzi wa kihasibu.

Aweso aliyasema juzi hayo katika mkutano na wakaguzi wa ndani, maofisa ugavi na watu wa fedha uliofanyika jijini hapa kwa lengo la kusikiliza kero wanazokutana nazo katika utendaji wao.

Waziri Aweso alisema Wizara ya Maji haina mashamba wala viwanja, hivyo hakuna haja ya kuwa na watumishi ambao ni madalali wa makandarasi na watoa huduma. Alisema mtumishi huyo anapaswa kusimamishwa ili asiendelee kuichafua wizara.

"Kaphipa anapaswa kusimamishwa kazi kwa sababu anaichafua Wizara kutokana na yeye kuhamishiwa Bonde la Tanganyika lakini bado anafanya kazi ya udalali katika wizara ilhali watendaji wa vitengo hivyo wapo,"alisema Aweso.

Alisema anahitaji kuona watumishi wanafanya kazi kwa weledi ili kuhakikisha vijijini na mijini watu wote wanapata maji.




Mwenyekiti mpya wa Baraza la Taifa la Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (NACONGO), Lilian Badi, akila kiapo cha utumishi mbele ya Wakili wa Kujitegemea, Deus Nyabiri, baada ya kuchaguliwa katika mkutano wa uchanguzi wa Baraza hilo, jijini Dodoma juzi. PICHA: PETER MKWAVILA

# DC ageukia mapambano dhidi ya corona

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

MKUU wa Wilaya ya Dodoma, Jabir Shekimweri, ameagiza masoko yote, stendi za mabasi, daladala na kwenye mikusanyiko kuhakikisha zinawekwa ndoo za maji tiririka na sabuni kwa ajili ya kujilinda na maambukizi ya corona.

Shekimweri alitoa agizo hilo jana alipokuwa akizungumza na wafanyabiashara wadogo (machinga) wa soko la Sabasaba jijini hapa.

Sambamba na hilo, pia aliagiza maeneo yote yenye mikusanyiko kama vile masoko, stendi za mabasi na daladala, kuwekwa ndoo za maji tiririka na sabuni.

"Ninaangiza viongozi ndani ya masoko, stendi za mabasi na daladala kuhakikisha ndoo za maji tiririka zinakuwapo pamoja na sabuni za kunawia mikono. Kwenye milango ya kuingilia na katikati hii ni pamoja na kwenye maeneo yenye mikusanyiko yote.

"Serikali imetangaza kujilinda na ugonjwa huo, hivyo tunatakiwa kuunga mkono katika kujihadhari pamoja na kuhakikisha tunakuwa wasafi huku tukivaa barokoa kila wakati kwenye maeneo ya mikusanyiko," alisema.

Pia aliwataka machinga kwenye masoko kuheshimu sheria zilizopo ambazo zimewekwa na Halmashauri ya Jiji, ikiwamo kutofanya biashara katika maeneo yasiyo rasmi ambayo yanayohatarisha maisha yao na usalama wa bidhaa zao.

Alisema machinga walio wengi wamekuwa wakifanya biashara zao bila utaratibu na kukiuka sheria hali ambayo imekuwa ikisababisha usumbufu mkubwa kwa watumiaji wa maeneo hayo.

Mbunge wa Dodoma Mjini, Anthony Mavunde, aliwataka machinga kuheshimu mipaka yao ya kufanyia biashara ili kuondokana na uharibifu unaoweza kujitokeza.

Mavunde alisema kazi ya umachinga ni kama nyingine, hivyo wanatakiwa kuheshimu na kutii sheria zilizowekwa.



HABARI ZANZIBAR

# Rais Mwinyi aonya ucheleweshaji mradi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amewataka makandarasi wa mradi wa maji wa Benki ya Exim kuelewa kuwa unapaswa kukamilika kwa wakati kama ulivyopangwa.

Dk. Mwinyi alitoa agizo hilo jana alipotembelea mradi wa Maji wa Exim Bank ulioko Dole, Wilaya ya Magharibi A, ikiwa miongonni mwa ziara yake ya kukagua shughuli za maendeleo na kusikiliza changamoto mbalimbali zinazowakabili wananchi.

Alisema pamoja na mradi huo kuchelewa kuanza kwa wakati, umekuwa na kasoro na urasimu katika utekelezaji wake.

Mradi huo mkubwa, alisema unaogharimu zaidi ya Dola za Kimarekani milioni 92.18 ni wa miezi 18, hivyo ni lazima ukamilike kwa wakati na kukabidhiwa serikalini muda uliopangwa utakapofika.

Alisema sababu zote zilizotolewa kukwamisha hatua ya kuanza mradi huo ni mambo yaliyo ndani ya uwezo wa watendaji wa mamlaka inayohusika.

Rais Mwinyi pia alitembelea visima vibovu eneo la Welezo pamoja na visima vya maji vilivyoko Bumbwisudi na kusema huduma za maji safi na salama zitapatikana ndani ya kipindi kifupi kijacho kupitia njia ya muda mfupi na muda mrefu.

Naye Mwakilishi wa Bububu, Mudrik Ramadhan Soraga, alisema mradi wa Exim Bank ni mwarobaini katika utatuzi wa tatizo la maji safi na salama, si tu kwa Jimbo la Bububu, bali kwa wilaya za Magharib A na B na Wilaya Kati Unguja.

Soraga ambaye pia ni Waziri wa Uwekezaji, alisema umuhimu wa serikali ni kuondokana na utaratibu wa kuwa na miradi mingi na kuchimba kisima kimoja na badala yake kuwa na mradi mmoja utakaohusisha uchimbaji wa visima vingi.

Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA), Dk. Salha Mohamed Kassim, alisema mradi wa maji wa Exim Bank unaolenga kuimarisha huduma za upatikanaji wa maji, unagharimiwa kwa fedha za mkopo kutoka Exim Bank ya India.

Dk. Salha Alisema mradi huo utahusisha uchimbaji wa visima 64 na matangi 14 ya maji.

Dk. Salha alizitaja sababu mbalimbali zilizofanya mradi huo ushindwe kutekelezwa kwa wakati uliopangwa kuwa ni pamoja na ufunguzi wa huduma maalum za malipo, kuchelewa kwa kibali cha ujenzi wa matangi ya maji, misamaha ya kodi na kusema rasilimali ya mchanga utakaotumika kwa ajili ya ujenzi wa matangi hayo itaagizwa kutoka Tanzania Bara.

Katika ziara yake hiyo katika Wilaya ya Magharib A na B Unguja, Dk. Mwinyi alipata fursa ya kutembelea Shule ya Abdalla Sheria Tomondo, kukagua mradi wa maji wa Exim Bank Kwarara Kidutani, Barabara ya Kibondeni, Mradi wa Maji wa Exim Bank Dimani pamoja na Mardi wa Maji wa Exim Bank Maungani.



Meneja wa Hoteli ya Park Hyatt Zanzibar, Nicolas Cedro (kulia), akizungumza katika uzinduzi wa chakula cha piza ndefu yenye futi 10, katika mgahawa wa Beach House, Mjini Unguja jana. PICHA: RAHMA SULEIMAN

# Mbunge asisitiza ubunifu kwa utalii

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MBUNGE wa Mpendae, Taufiq Salum Turky, amesema ni muhimu kuwa na ubunifu katika kukuza utalii wa Zanzibar ambao utasaidia kuitangaza sekta hiyo na Zanzibar kupata wageni wengi.

Aliyasema hayo jana katika hafla ya uzinduzi wa upishi wa pizza ndefu Tanzania yenye urefu mita 10 iliyopikwa na Hoteli ya Park Hyatt kupitia mgahawa wa Beach House, Shangani Mjini Unguja.

Alisema upishi huo umewavutia wageni wengi waliopo katika mgahawa huo ambao umechangia hoteli hiyo kuongeza kipato.

"Ubunifu kama huu ni jambo zuri sana unachangia kuutangaza utalii wa Zanzibar na kama unavyoona leo (jana) hapa watu wamejaa kushuhudia uzinduzi wa upishi huu wa piza ndefu," alisema.

Turky alisema katika kukuza utalii, hakuna kuridhika watalii kutembelea vivutio vya utalii pekee bali kuwa na ubunifu wa ziada ili kupata faida zaidi.

Mbunge huyo alizitaka hoteli zingine kuwa wabunifu ili kuwavutia watalii kwa sababu watalii wanapenda kuona vitu vipya ambavyo nchini kwao havipo.

Naye Meneja wa Park Hyatt Zanzibar, Nicolas Cedro, alisema lengo la kuandaa upishi huo ni kukuza utalii wa Zanzibar na kuwavutia wageni wanaofika Zanzibar.

Alisema kuwa upishi huo wa piza ndefu umewakutanisha watu wa mataifa mbalimbali kujionea na kula chakula hicho ambacho kimenogeshwa na viungo vya Zanzibar.

Baadhi ya wageni waliofika katika mgahawa huo, walisema upishi huo wa piza ndefu ni mara ya kwanza kuuona na umewavutia sana.

# Ataka vibali kuepusha ujenzi holela

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

DIWANI wa Wadi ya Magogoni Unguja, Fatma Juma Jabu, amewataka wakazi wa wadi hiyo kufuata utaratibu wa kukata vibali vya ujenzi ili kuepusha ujenzi holela.

Akizungumza na wananchi wa shehia ya Mikarafuuni jana, Fatma alisema mazingira ya shehia hiyo hayako salama kutokana na ujenzi holela, hivyo kusababisha uchafuzi wa mazingira na maradhi ya mlipuko.

Suala la ujenzi salama, alisema ni muhimu hivyo wananchi lazima wazingatie usafi katika maeneo yao na kuacha kutupa taka ovyo ili kujikinga na madhara yanayoweza kutokea kutokana na ujenzi holela uliokithiri katika shehia hiyo.

Pia alisema ujenzi holela unachangia uchafuzi wa mazingira kutokana na kujenga nyumba zisizo na mpangilio na kusababisha kuziba njia za majitaka na kuibuka madhara hasa kipindi cha mvua.

Naye Sheha wa Shehia hiyo, Suleiman Haji Ali, aliwataka wananchi kuacha kumwaga maji machafu na badala yake kujenga makaro ambayo yatahifadhi maji hayo.

Alisema Shehia ya Mikarafuuni inakabiliwa na wimbi la vitendo viovu ikiwamo matumzi ya dawa za kulevya na wizi jambo ambalo linasababisha kukosa nguvu kazi ya taifa.

Kuhusu ulinzi katika Shehia hiyo, alisema tayari ameshazungumza na wananchi kujitokeza kwa vijana kujiunga katika vikundi vya ulinzi shirikishi ili kudhibiti vitendo viovu.

Nao wananchi wa shehia hiyo, walisema ukosefu wa uzio katika Shule ya Magogoni unasababisha kukithiri kwa vitendo viovu ikiwamo udhalilishaji jambo ambalo linahatarisha maisha ya wanafunzi.

Nipashe
MWANGA WA JAMII
BT
BURUDANI TELE
JUMAMOSI JULAI 10, 2021



MTOTO WA WIZKID MOTO MKALI Uk.14



## HAMKANI SI SHWARI

# Mbosso, Aslay wazidi kutunishiana

NI wazi kuwa sasa wasanii waliounda kundi la Yamoto Band, hawana maelewano tena baada ya kugawanyika makundi mawili.

Wasanii hao Aslay, Beka Flafour, Enock na Mbosso, walitawanyika baada ya kundi hilo lilopata umaarufu nchini, kuvunjika na kila mmoja kuamua kufanya kazi kivyake.

Uvuni kwamba wanamuziki hao hawaelewani hasa Aslay na Mbosso, umeanza siku nyingi lakini siku zinavyozidi kusonga mbele tofauti zao zinazidi kuonekana wazi.

Hata hivyo, wote wamekana kuwa na tofauzi na badala yake wanasema wapo wamoja Ikama ilivyo zamani.

Hata hivyo, katika tukio la hivi karibuni Aslay na Mbosso, walikacha kufika katika sherehe ya kuzaliwa msanii mwenzao, Beka Flavour, huku kila mmoja akidai kubanwa na kazi.

Baadhi ya wachambuzi wa sanaa wanasema, wasanii hao wamegawanyika kutokana na mvutano huo, kiasi ambacho imekuwa vigumu kwa sasa kurudi katika maisha yao ya zamani ya kuwa kama ndugu.

"Ugomvi wa Aslay na Mbosso, umesababisha kuwatenga kabisa Beka na Enock, hawa wanajikuta wakifuata upepo tu, hawana nguvu ya kuwapatanisha na ndio maana hata kwenye sherehe wote walishindwa kufika," alisema mwanamuziki mmoja ambaye hakutaka jina litajwe.

Kwa upande wa Beka, ametetea kukosekana kwa wanamuziki hao, akisema imetokana na yeye kuandaa pati hiyo kwa kukurupuka na si kuna tofauti kati yao.

"Niliandaa sherehe hii kwa kukurupuka, niliwaambia washkaji zangu kwamba nina pati yangu ya siku ya kuzaliwa kwangu, lakini wakaniambia wana mambo kidogo watashindwa kuja," Beka.

BASI SAWA

## Roma Mkatoliki hakamatiki You Tube



TANGU kuanza kupendwa kwa muziki wa Hip Hop, wasanii wake walionekana kama wahuni na wasio na mwelekeo, lakini sasa hali imekuwa tofauti baada ya waimbaji hao kuwa na ushindani mkubwa wa mafanikio.

Kama ishara ya kupata mafanikio, mtandao wa EATV, umechapisha majina ya marapa ambao wana watazamaji wengi katika mtandao wa YouTube na Roma Mkatoliki, ameibuka kinara kuwa na mashabiki zaidi ya milioni 35.

Waliofuata katika orodha hiyo ni, Professor Jay, mwenye watazamaji milioni 27, Fid Q milioni 10.2, Country Wizzy milioni 8.1 na Joh Makini ana milioni 8.

## Harmonize huyooo Marekani



MAMBO yanazidi kuwa mazuri kwa mwanamuziki Harmonize, ambaye ametangaza ziara yake ndefu ya kikazi nchini Marekani.

Kupitia ukurasa wake wa Instagram, Harmonize, ameweka wazi kwamba atakaa huko kwa miezi miwili akiwatumbuiza mashabiki wake katika majiji tofauti.

Hii itakuwa ziara yake ya kwanza kutumia muda mrefu nje ya nchi kwa ajili ya kikazi.



## Recho azimia mapenzi ya wahuni

UKISIKIA kituko ndio hiki, unaambiwa mwanamuziki Recho Kizunguzungu, haambiwi kitu kuhusu wanaume wahuni, warefu na weupe.

Kiujumla yeye akiomuona mwanamume mstaarabu na mtulivu, kwake linamchefua na hawezi kumsogolea hata kidogo.

"Sijawahi kupenda mwanamume mweusi, napenda wanaume weupe, warefu, wawe wahuni wahuni fulani hivi, utofauti wao naweza kuujua mwenyewe kipindi ninapokuwa naye huko ndani, hizo sifa siwezi kumwambia mtu yeyote kwa hiyo sifa zao ninazo mimi mwenyewe na na-enjoy kumuona" amesema Recho Kizunguzungu.



## Aunty Ezekiel ambeba Wema

KAMA uliona Aunty Ezekiel atamponda Wema Sepetu, kutokana na kitendo chake cha kutangaza tiba ya mitishamba, basi utakuwa umekosea.

Aunty Ezekiel, hakusita kusema rafiki yake huyo wa karibu hakufanya kosa lolote, kwani watu watambue nyumba ya ustaa kuna maisha na wanatakiwa kuhangaika kupata mlo wa kila siku.

Amenena hayo baada ya baadhi ya mashabiki katika mtandao wa Instagram kumshambulia Wema Sepetu, baada ya kuposti matangazo hayo huku wakidai anashusha brandi yake.

"Mimi nadhani ifike muda watu wajue kuna maisha baada ya ustaa, mtu anaona kuna fursa ya kufanya kitu na akapata pesa kwanini asifanye kwa sababu hata yeye ni binadamu kama walivyo wengine, wanaongea wanaona yao yamekwama wamuache afanye matangazo sidhani kama ni shida" amesema Aunty Ezekiel

## Mtoto wa mwenzako ni wako

**Na Adam Fungamwango**

KUNA baadhi ya wanawake wana dhana kuwa mtoto ili awe wa kwake ni lazima awe amemzaa yeye. Anapoolewa na kwenda kwa mume akakuta watoto wengine anawachukulia kama si watoto wake.

Na kwa bahati nzuri Mungu akimjalia kupata watoto kwenye nyumba aliyoolewa ndiyo kabisa, watoto aliowazaa ndiyo wanawapa kipaumbele.

Ndani kuwa na watoto wa daraja la kwanza na wengine wa daraja la chini. Hii mara nyingi kuleta chuki na mateso makubwa na kubaguana.

Wakati mwingine hali hii inakwenda na kuwa sugu hadi ukubwani, watoto wanakuwa hawaelewani maisha.

Filamu na 'Haki ya Mtoto', inakumbusha kuwa na ni wajibu wa mwanamke au mwanaume, akioa au kuolewa na kumkuta mwenza ana watoto awalee na kuwachukulia kuwa ni watoto wake pia.

Imechezwa na wasaniii Robert Ruta, Kessy Said, Treasure Samson, Chiku Sada na wengineo.

Inaanza kumwonyesha Mama Juma, akichapa mtoto wa kike. Binti huyo mdogo wa darasa la tano anaitwa Moureen. Mama yake alifariki dunia. Baba yake Kessy akaona mke mwingine. Ndiyo huyo mama Juma. Wakazaa mtoto anaitwa Juma. Mama akaona hapo sasa urithi sasa utakwenda kwa mwanaye Juma.

Kilichoanza hapo ni manyanyaso kwa Maoureen. Anaanza kunyimwa chakula, anapigwa bila sababu za msingi, anafungiwa chooni, akatukanwa na kushindishwa kwenye pango , akifanyika kila aina ya ukatili.

Kibaya zaidi alikuwa hataki aitwe mama kwa sababu eti mama yake yuko kaburini. Alimwambia Moureen amwite mke wa baba.

Mpenzi yanampofusha Kessy. Kila anapoambiwa jirani zake, anaona ni kama wanataka kuliangamiza penzi lake. Hata mjumbe alipopelekewa mashtaka, kassy alikwenda kumhonga pesa ili aachane na jambo hilo.

Mtoto aliteswa na kuteseka. Mahudhurio na maendeleo shuleni yalianza kushuka. Yote tisa, kumi sasa akaamua amuue kabisa. Siku hiyo tumbo mtoto lilimuuma. Badala ya dawa akapewa sumu. Wakati huo akiwa anataka kwenda shuleni. Akiwa huko tumbo lilimzidia na kukimbizwa hospitalini. Majibu ya daktari wakasema msichana alikunywa sumu. Taarifa zikatapakaa. Maoreen baada ya kupona akalimwaga hadharani kuwa alinywesha sumu na mama yake wa kambo.

Majirani wakaona isiwe tabu. Wakaungana na kwenda kushtaki polisi. Mama Juma akakamatwa.

Pamoja na Kessy kutaka kwenda kuhonga polisi, juhudi zake zinagonga mwamba. Akiwa kifungoni ndipo mama Juma anaanza kujuta ni kwa nini alimtesa mtoto huyo.



## Mwendo wa Singeli mpya

**Na Adam Fungamwango**

SIKU hizi mambo ni singeli bwana. Hivyo ndivyo wanavyosema watoto wa uswahilini maarufu kama uswazi. Ni kweli muziki wa singeli ambao awali ulikuwa kama haueleweki hivi na ulionekana ni wa kihuni, umeonekana kushika chati kwelikweli.

Imefikia wakati hata wasanii wengi maarufu wa bongo fleva wameanza nao kujikita huko na kutoa mara moja moja ngoma zenye mahadhi ya singeli ambayo ni mchangayiko wa ngoma za kizaramo, mnanda na mduara.

Mwezi uliopita na huu, zimetoka ngoma ambazo tayari zimeanza kuvuta hisia kwa mashabiki wa muziki huo. Hebu tuziangalie ngoma hizo ambazo kwa muda mfupi tu tangu zitoke zimeanza kuwa gumzo.

**Nyumba Ndogo-Zuchu**

Kama nilivyosema hata wasanii wa bongo felva siku hizi wamo kwenye singeli. Msanii Zuchu Julai Mosi ametoa ngoma yake mpya iitwayo 'Nyumba Ndogo' yenye mahadhi ya singeli.

Kwenye pini hiyo, Zuchu anawasilisha maudhui ya baadhi ya wanawake hasa wa uswazi. Kuna baadhi ya wanawake huko kazi yao kuchukua mabwana na waume za watu,wao wanasema kizuri kula na mwenzako.

Kuna dada anajitambulisha kwa mwanamke mwenzake kama yeye ni nyumba ndogo. Anamsuta mwenzake yeye anampa vitu vyote ambayo mume wake havipati kwake.

Halafu anampoza kuwa hana ubaya na yeye, ila ajitahidi tu asiachike. Unaweza ukadhani kama Zuchu anaimba vitu vya kufikirika. Lakini uliza yoyote anayekaa uswazi, atakusimulia zaidi ya Zuchu anavyoimba singeli hiyo.

**Jambo la Kheri-Dulla Makabila**

Mzee na singeli, Dulla Makabila, kama kawaida yake yeye ametoka na ngoma mpya aliyoiita, 'Jambo la Kheri.'

Kwenye ngoma hii, Dula analalamika na kuwachana baadhi ya watu ambao wao ni rahisi sana kumletea kadi za mwaliko ili achangie pesa, lakini yeye alipotaka kuona na kuomba achangiwe, wale wote ambao aliwachangia walimzimia simu. Ngoma hii ameitoa Juni 20.

**Stress-Balaa MC**

Msanii huyo ambaye kwa sasa amebamba sana kwenye sanaa hii, Juni 24 amekuja na ngoma moja kali inayoitwa 'Stress'.

Kwenye pini hii yanaelezwa mambo mbalimbali yanayomfanya kuwa na mawazo. Mtu alichwa na mwanamke atakuwa na stress, akidaiwa kodi atakuwa na stress na hata akivurugwa tu na maisha ni lazima atakuwa nayo.

**Machanganyiko-D Voice ft Baddest 47**


Unamkumbuka yule aliyeimba 'Nikagongee?' Yumo kwenye ngoma ya singeli akiwa ameshirikishwa na msanii mmoja hivi wa singeli anaitwa D Voice.

Huu ni wimbo wa mapenzi, ambapo jamaa anamsifia mpenzi wake, akitaja vitu ambavyo anaamini vimefanya kumpenda. Ngoma imetoka Juni 28.

Demu Wangu-Bright Ft Meja Kunte

Sikukuu ya Sabasaba umetoka wimbo ulitwao 'Demu Wangu' ambao ni wa msanii Bright akimshirikisha mmoja wa wasanii maarufu wa muziki wa singeli, Meja Kunte.

Pia huu ni wimbo wa mapenzi.
mwisho





# Stella hadi 'kung fu' ya kichina!

MWIGIZAJI mkongwe kutoka Nollywood, Stella Damasus, amewashauri wanawake kujifunza sanaa ya mapigano kwa ajili ya kujilinda na manyanyaso kutoka kwa wapenzi wao.

Staa huyo wa filamu, ametoa ushauri huo baada ya kuchangia video fupi iliyowekwa na shabiki yake katika mtandao wa Instagram, ikimuonyesha mwanamama mmoja akimpiga mumewe baada ya kutoka nje kimapenzi.

"Kwangu naona video inahamasisha wanawake kujifunza sanaa ya mapigano kwa ajili ya kujilinda dhidi ya unyanyasaji kutoka kwa wanaume," amesema Stella.



## Wolfe, Jodi kupeana talaka

HALI inazidi kuwa mbaya kwa wanandoa mastaa wa Marekani, baada ya mke wa mchekeshaji maarufu Michael Wolfe, kufungua kesi ya madai ya talaka.

Jodi Catherine Wolfe, alifungua kesi hiyo katika mahakama ya nyumbani kwao Williamson, jimbo la Tennessee baada ya kuishi katika ndoa kwa muda wa miaka 10.


Wawili hao walifanikiwa kupata mtoto mmoja wa kike mwenye umri miaka tisa, huku kila mmoja akitaka kuwa na haki ya kumlea.

## Wengi wamlilia Obama DMW

WASANII mbalimbali wanaendelea kuomboleza kifo cha mwanamuziki nyota, Obama DMW, ambaye alifariki ghafla kutokana na matatizo ya moyo.

Obama alifariki jumanne ya wiki hii katika hospitali ya Lekki, iliyoko jijini Lagos, baada ya moyo wake kushindwa kufanya kazi.

Mwanamuziki mkali nchini humo, Davido, ambaye alikuwa rafiki yake wa karibu, ameeleza ameshtushwa na kuhuzunishwa na kifo cha mtu wake wa karibu na kamwe anaona kama bado yupo naye karibu.





## Mtoto wa Wizkid moto mkali

MTOTO wa mwimbaji nyota nchini Nigeria, Wizkid, ameibua majadala katika mitandao ya kijamii baada picha yake kuonekana kivutio kwa mashabiki wengi.

Zion ni mtoto wa tatu wa Wizkid, alitupia picha yake katika mtandao wa Instagram, akiwa amevaa fulana ya shati ya rangi nyekundu na suruali ya bluu.


Mashabiki hao walimwagia sifa mtoto huyo na kumuelezea kama staa mwingine anayechipukia nchini humo.

## Burna Boy hanaga kuremba

MWANAMUZIKI kutoka Nigeria, ameamua kufanya kweli na sasa anajiandaa kuachia Albam yake mpya, baada ile ya 'Twice as Tall' kumpa mafanikio.

Mshindi huyo wa Grammy na BET, amesema kazi hiyo itakuwa hadharani Agosti 14, mwaka huu.

Album hiyo itakuwa ya sita, huku ikilezwa kuna mastaa kibao kutoka Marekani kama Sean Love Combs (P. Diddy) ambaye atakuwa mtayarishaji mkuu.





# Wizara ya Mifugo na Uvuvi inapojivunia siku 100 ya Rais Samia Suluhu Hassan

**Na Moshi Lusonzo**

WIZARA ya Mifugo na Uvuvi, imejizatiti kutekeleza mikakati ya kuhakikisha serikali na wananchi wananufaika moja kwa moja na uzalishaji wa mazao na bidhaa inayotokana na sekta hizo.

Mkakati huo umewekewa mkazo baada ya Rais Samia Suluhu Hassan, kuingia madarakani na matunda yake yameanza kuonekana ikiwamo kuongezeka kwa mapato yatokanayo ya shughuli ya ufugaji na uvuvi wa bahari na kwenye maziwa makuu.

Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, anasema kazi hizo ni zile zilizopangwa kutekelezwa katika mwaka wa fedha 2020/2021, na kuwekewa mkazo ndani ya siku 100 ya serikali ya awamu ya sita.

Waziri Ndaki, anasema baadhi ya kazi hizo zimetokana na maelekezo ya Rais Samia Suluhu Hassan, aliyoyatoa katika matukio mbalimbali ili kuboresha sekta za mifugo na uvuvi.

**UTEKELEZAJI KATIKA SEKTA YA MIFUGO**

Katika kipindi cha siku 100 ya Serikali ya awamu ya Sita, mafanikio yaliyopatikana katika sekta ya mifugo ni mengi, lakini kwa kiasi kikubwa ni kuendeleza miundombinu ya ufugaji na kuboresha masoko.

Waziri huyo anasema katika kipindi hicho, Wizara imechimba visima virefu viwili katika Halmashauri ya Wilaya ya Iringa eneo la Usolanga na Mpapa Halmashauri ya Manyoni.

Pia, anasema wamekarabati mabwawa matatu ya Chamakweza halmashauri ya Chalinze, Kimokoua (Longido) na Narakauo (Simanjiro), na kazi imekamilika kwa asilimia 100.

"Tumetenga hekta 32,044.21 katika Wilaya za Tanganyika, Nsimbo na Mlele kwa ajili ya malisho ili kuongeza thamani mifugo yetu," anasema Waziri Ndaki.

Ili kuboresha bidhaa ya mifugo, wizara hiyo imetoa mafunzo na kutoa leseni kwa wachunaji ngozi 340 wa machinjio za Manispaa ya Kinondoni na Temeke jijini Dar es Salaam.

"Pamoja na mafunzo hayo, tumewapatia vitendea kazi wakaguzi wa Ngozi 34 wa Wilaya za Mikoa ya Mwanza, Simiyu, Shinyanga na Mara. Lengo ni kuwezesha upatikanaji wa ngozi bora kwa ajili ya viwanda vyetu vya ndani na nje ya nchi," amezidi kueleza.

Katika kuongeza kasi ya biashara na kuwapatia wafugaji kipato, serikali imefungua mnada wa mifugo wa mpakani wa Magena, mkoani Mara ili kuwezesha biashara ya mifugo kati ya Tanzania na Kenya kuendelea. Pia, ujenzi wa mnada wa mifugo wa upili wa Buzirayombo, mkoani Geita umefikia asilimia 50.

Aidha, jumla ya ng'ombe wa asili 197 katika mikoa ya Iringa walifanyiwa uchambuzi ili kubaini na kutunza mbari za asili.

**USHIRIKIANO NA ZANZIBAR**

Waziri Ndaki, anasema katika kipindi hicho Wizara ya Mifugo na Uvuvi upande wa mifugo, na Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo kwa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ) zimefanya kikao na kukubaliana kuendeleza ushirikiano kiutendaji katika ngazi za idara na taasisi zilizo chini ya Wizara hizo. Lengo ni kuimarisha sekta za mifugo katika pande zote mbili za muungano ili ziweze kuchangia zaidi katika ukuaji wa uchumi na maendeleo ya wananchi.

**SEKTA YA UVUVI**

Sekta ya Uvuvi ni moja kati maeneo yanayokuwa kiuchumi kwa haraka hapa nchini. Shughuli za uvuvi huchangia katika kuwapatia wananchi uhakika wa chakula, lishe, kuongeza kipato na kupunguza umaskini.

Kutokana na umuhimu wake, serikali imekamilisha ujenzi wa majengo matatu ya ofisi kwa ajili ya vikundi vya Usimamizi wa Rasilimali ya Uvuvi (BMU) katika Wilaya za Pangani katika kijiji cha Kipumbwi, Mkinga kijiji cha Zingibari na Bagamoyo kijiji cha Dunda.

Katika maeneo ya maziwa, wizara imeboresha miundombinu wezeshi uvuvi kwa kuanza ujenzi wa mialo sita katika kanda ya ziwa Victoria, ujenzi wa soko la samaki la Mbamba Bay-Nyasa Mkoani Ruvuma, na kutangazwa kwa zabuni ya kupata Mkandarasi wa Ukarabati wa Soko la Samaki la Feri, jijini Dar es Salaam utakaoanza mwezi Julai, mwaka huu.

Pia, imetengwa Sh. bilioni 50 katika bajeti ya 2021/2022 kwa ajili ya kuanza ujenzi wa Bandari ya Uvuvi katika eneo la Mbegani Wilaya ya Bagamoyo.

"Kanuni mpya za kusimamia na kuendeleza uvuvi wa bahari Kuu zimetayarishwa na kutangazwa katika Gazeti la Serikali Na. 334 tarehe 23 Aprili, mwaka huu, yote haya ni kwajili ya manufaa ya wananchi ", amezidi kusisitiza Waziri Ndaki.

**FURSA ZA UWEKEZAJI**

Serikali imetangaza fursa za uwekezaji zilizopo kwenye Sekta ya uvuvi kupitia mikutano mbalimbali ya kitaifa iliyojumuisha wageni kutoka nje.

Nchi zilizoshiriki ni Ufalme wa Saudi Arabia, China na Umoja wa Falme za Kiarabu.

Mikutano hiyo ilipelekea kwa mara ya kwanza Mamlaka ya Kusimamia Uvuvi wa Bahari Kuu (DSFA) kukusanya jumla ya dola za Marekani 800, 000 sawa na Sh. bilioni 1.84 kama malipo ya leseni za uvuvi wa Bahari Kuu kwa meli 22.

Mafanikio hayo yamepatikana baada ya meli za kigeni kusitisha kuchukua leseni za Tanzania kuanzia mwaka 2017 kulikosababisha serikali kukosa mapato na DSFA kushindwa kujiendesha.

"Katika kuhakikisha hakuna meli inayosumbuliwa, tumenunua boti 12 na injini sita za kupachika kwa ajili ya kuimarisha ulinzi wa rasilimali za uvuvi," anaongeza kusema.

Aidha, DSFA ilikamilisha maandalizi na kuwezesha mawaziri wenye dhamana ya Sekta ya Uvuvi pande mbli za muungano kusaini kanuni mpya za kusimamia na kuendeleza Uvuvi wa Bahari Kuu za mwaka 2021 na kuanza kutumika rasmi Aprili 23, mwaka huu.

Ili kunufaika na fursa za Uchumi wa Buluu kupitia tasnia ya ukuzaji viumbe maji, Serikali imetenga Sh. bilioni 18 ambazo zitatumika kujenga, kukarabati na kupanua miundombinu katika vituo sita vya kuendeleza ukuzaji viumbe maji vya Mwamapuli mkoani Tabora, Ruhila (Ruvuma), Kingolwira (Morogoro), Nyengedi (Lindi), Machui (Tanga), na Rubambagwe mkoani Geita.

Katika mkakati huo mashamba darasa 40 ya ufugaji samaki yatayosimamiwa na vikundi vya vijana na kinamama. Huu ni mwanzo wa utelekezaji wa azma ya kuwa shamba darasa katika kila halmashauri nchini ili kuhamasisha ufugaji wa samaki nchini kwa ajili kuboresha lishe, kuongeza kipato na kukuza uchumi wa wananchi wa kawaida.

Aidha, ili kuhamasisha umefanyika wa ukuzaji viumbe maji bahari, wakulima wa mwani katika maeneo ya Mkinga mkoani Tanga na Mchinga mkoa wa Lindi. Pia wafugaji wa majongoo bahari wilaya ya Bagamoyo wamenunuliwa vitendea kazi vyenye thamani ya shilingi 15,000,000.00 ili waweze kuongeza uzalishaji.

MAKALA

## POULO MWETA

# Kijana mwenye uhitaji maalum anayepambana kujitegemea

**Na Christina Mwakangale**

“NILIANZA darasa la kwanza nikiwa na miaka 15 pekee, kutokana na tatizo nilikuwa nalo tangu kuzaliwa, nilipokuwa mkubwa nikaanza kubeba mizigo ya watu, kuchota maji na kulipwa ujira mdogo ili kujikimu.”

Ni simulizi ya Paulo Mweta, kijana ambaye anaishi akiwa na matatizo katika mfumo wa ukuaji wake na kusababisha kuishi katika kundi la watu wenye uhitaji maalumu.

Mweta, kutokana na mengi aliyopitia anaomba jamii iachane na imani potofu kwamba wenye watu wenye uhitaji maalum hawana talanta yeyote, bali ni mzigo na wasio na msaada wowote.

Akizungumza na Nipashe kwenye Maonyesho ya Biashara Kimataifa Dar es Salaam (DITF), kwenye bando la VETA, maalumu kwa kundi hilo, amesema kutokana na tatizo lake amepoteza uelewa wa masomo ya darasani, kiasi cha shule za msingi aina tofauti za umma na binafsi alizosoma, hazikumsaidia kupata ufumbuzi wa maisha yake ya baadae.

Paulo ambaye amezaliwa mwaka 1992, Tabata mkoani Dar es Salaam, anasema bado anaishi na wazazi wake kutokana na hali aliyokuwa nayo, huku akiwa na ndoto kubwa za kuzitekeleza maishani.

Kijana huyo ambaye tangu mwaka 2015, amejiunga na mafunzo kutoka Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi, (VETA), anasema kozi anayosomea ni ndefu na endelevu.



Kijana Paulo Mweta, akionyesha bidhaa ambazo amezitengeneza. **PICHA ZOTE: CHRISTINA MWAKANGALE**



Mwalimu Kintu Kilanga akielezea jambo kuhusu elimu ya kuwaendeleza wenye uhitaji maalumu ikiwamo wenye ulemavu katika banda la Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi, (VETA), Sabasaba, mkoani Dar es Salaam.

“Nilitamani kusoma lakini kila nikisimama nilikuwa naanguka, nimetibiwa sana Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), nimekwenda kwenye maombi nimefanyiwa na kuna wakati hata tiba ya kienyeji nilitumia lakini sikupata nafuu,” anasema Paulo.

Anasema katika familia yao ya watoto 10, yeye pekee alikumbwa na tatizo hilo tangu alipozaliwa na kwamba alipokwenda kuandikishwa masomo ya awali ilimbidi akae chini kwenye mkeka aweze kuandika vizuri.

“Nimesoma shule nyingi za msingi mara nisome niache, nianze tena tena, zingine za kulipia baba alinilipia lakini sikufanya vizuri. Hata darasa la saba niliambiwa nimefeli. Basi wazazi wangu hasa mama ambaye ni mwalimu mstaafu walinishauri niende VETA,” anasema.

Anaongeza “Waliniambia watu kama sisi inachukua muda mrefu kufanya kitu. Wakasema nenda katika ufundi, sikukubali mara moja, nilipomaliza darasa la saba nikawa nafanya kibarua kubeba mizigo,” anasema Paulo.

Anasema mara kadhaa jamii huwatenga watu kama yeye wakiwaona hawawezi kufanya kitu. Alipohitimu masomo yake ya elimu ya msingi shule ya Uhuru Mchanganyiko, jijini Dar es Salaam, akiwa tayari mtu mzima, alijiona akiwa na wazo la kuwa mjasiriamali.

“Wazazi walionipeleka VETA, waliniambia nisomee ujuzi ambao utanifanya niishi. Kuna wakati baba alisema wakiondoka duniani nitapata tabu bila kuwa na kitu cha kufanya. Niliwajibu wakati wa Mungu kusoma bado, ila mwishowe nikaamua kujifunza,” anasema kijana huyo.

Paulo, anasema hivi sasa ana uwezo wa kutengeneza bidhaa tofauti kwa kutumia chuma au mabati, kama vile majiko, vizoleo, majalo, mabanio na bampa za magari.

Anaeleza akishatengeneza hutembea katika maeneo tofauti kutafuta wateja.

“Zamani pesa niliyopata niliweka katika kibubu cha chuma nilichotengeneza, nikaona bora nitunze benki ili inisaidie nikiwa na tatizo. Huwa najitangaza serikali za mitaa na taasisi kujua ninauza nini ila tatizo ukimtajia mtu bei, kifaa Cha Sh. 5,000 yeye anasema niunzie 2,000 mteja anajipangia bei hajui vyuma ghali, ila sikatai pesa,” anasema Paulo.

Mbali na kutamani kukuza kipaji, Paulo hakusita kuelezea matumaini yake ya kuwa na mke, akitaja sifa zake ni lazima awe mwanamke mwenye heshima, asiye na dharau wala kejeli na kukubaliana na hali yake.

“Natamani nioe ila mke akubaliane na hali yangu niliyonayo asinidharau, sipendi dharau, aridhike hivi nilivyo.” anasisitiza

**MKUFUNZI**

Mwalimu wa watu wenye uhitaji maalumu kutoka VETA, Kintu Kilanga, anasema mwanafunzi kutoka kundi hilo wakifika chuoni hapo hufanyiwa tathmini kubaini kiwango chake cha ubunifu na kipaji alichonacho, ili kumpa maelekezo sahihi.

“Nilianza kufundisha tangu mwaka 2012, hivi sasa nina wanafunzi kadhaa wenye mahitaji maalumu wanaweza kutengeneza bidhaa za vyuma wenye na kinachopatika kifedha baadhi hufanikiwa kujikimu kimaisha,” anasema mwalimu huyo,” anasema.

Anashauri jamii kutokana na watoto wenye kundi hilo nyumbani badala yake wawapeleke shuleni na vyuo vya ufundi ikiwamo VETA, ili kugundua vipaji na kwamba serikali iandae walimu zaidi ambao wana ujuzi wa kutoa mafunzo maalumu.

# DRC sharti mgombea urais wazazi wake wawe wazawa

**Kinshasa, DRC**

MUSWADA uliowasilishwa katika bunge la Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo (DRC), utapelekea sheria za uraia kwa rais wa nchi hiyo kuwa kali zaidi na kumuondoa moja kwa moja katika kinyang'anyiro cha kuwania uongozi wa nchi hiyo, Moise Katumbi anayenuia kugombania urais.

Aliyekuwa mgombea wa urais mwaka 2018, Noel Tshiani ambaye ndiye aliyewasilisha muswada huo ameliambia shirika la habari la Ufaransa AFP kuwa, muswada wake unalenga kuiweka nafasi ya urais wa Congo iwe tu kwa raia ambao wamezaliwa na wazazi wawili wenye uraia wa nchi hiyo.


Tshiani ni rafiki wa karibu wa rais wa sasa Felix Tshisekedi na wote wanatokea eneo la Kasai.

Tshisekedi tayari ameshaonyesha nia yake ya kugombea tena kiti hicho katika uchaguzi ujao.

Kambi ya Katumbi ilisema gavana huyo wa zamani wa jimbo la Katanga ameukosoa muswada huo.

Mamake Katumbi ni raia wa Congo ila babake ni Mgiriki.

**DW**



# Zuma huenda kusamehewa baada ya miezi minne jela

**Johannesburg, AFRIKA KUSINI**

WAZIRI wa Sheria wa Afrika Kusini, Ronald Lamola, amesema rais wa zamani wa nchi hiyo, Jacob Zuma ambaye ameanza kutumikia kifungo chake cha miezi 15 jela, anaweza kustahiki msamaha na kuondoka jela baada ya miezi minne.

Waziri Lamola amewaambia waandishi wa habari kuwa, Zuma atawekwa karantini kwa siku 14 kuzingatia kanuni za kupambana na ugonjwa wa Covid-19.

Aliongeza kuwa chini ya kanuni za idara ya magereza za Afrika Kusini, Zuma atastahiki kupata msamaha mara baada ya kutumikia robo ya muda wa kifungo chake.

Aidha Lamola alisema Zuma atalindiwa heshima yake katika kipindi chote atakachokaa gerezani.

Rais huyo wa zamani wa Afrika Kusini mwenye umri wa miaka 79, alijisalimisha mwenyewe usiku wa kuamkia leo kwa polisi na kupelekwa gereza la mkoa wa KwaZulu-Natal.

Chama tawala cha Afrika Kusini cha African National Congress (ANC), ambacho kiliwahi kuongozwa na Zuma, kilisema katika taarifa kuwa kinaheshimu uamuzi wake wa kutii sheria; na kwamba ni jambo la ujasiri na uamuzi mgumu.

DW



Pichani Gari lilomchukua Rais wa zamani wa Afrika Kusini, Jacob Zuma, likielekea gerezani baada ya kiongozi huyo kujisalimisha kwa polisi ili kutumikia adhabu ya kifungo cha miezi 15 jela, huku baadhi wananchi wakishangilia: **PICHA: BBC**

# 'Afrika ijiandae hali mbaya zaidi wimbi la tatu corona'

SHIRIKA la Afya Duniani (WHO), limetahadharisha hali mbaya zaidi ya ugonjwa wa corona itashuhudiwa barani Afrika, huku mataifa mengi yakikabiliana na aina ya corona inayofahamika kama Covid-19 Delta inayoendelea kusambaa.

WHO imezitaka nchi za Afrika kuzingatia hatua za usalama, huku zikijiandaa kwa mpango mpya wa utoaji wa chanjo kwa ajili ya kukabiliana na virusi.

WHO inasema kuwa wiki ya mwisho ya mwezi Juni ilikuwa ni wiki mbaya zaidi kwa maambukizi katika bara la Afrika.

Mkurugenzi wa Kanda ya Afrika Dk. Matsidisho Moeti alisema kuwa maambukizi mapya ya corona yanaongezeka maradufu kila baada ya siku 18.

Ongezeko kubwa la wimbi la tatu la maambukizi linaweza kutokea wiki chache zijazo.

Katika baadhi ya nchi, kama vile Namibia na Tunisia, hospitali zinahangaika kukabiliana na idadi kubwa ya wagonjwa.

Huku chini ya asilimia mbili ya watu wakiwa ndio waliopata chanjo kamili, wengi wataendelea kukabiliwa na hatari ya kuugua corona.

WHO ina matumaini kwamba misaada kutoka Marekani na nchi nyingine kupitia mpango wa usambazaji wa chanjo Covax utasaidia nchi kuinua kampeni za chanjo.

**BBC**

# Polisi: Kikundi cha kukodi kilitekeleza mauaji rais Moise

**Port-au-Prince, HAITI**

KIKOSI cha mauaji kinachoundwa na askari wengi wastaafu wa Colombia, kinatajwa kuhusika katika mauaji ya Rais wa Haiti, Jovenel Moise, yaliyotokea wiki hii, Polisi imesema.

Kwa mujibu wa Mkuu wa Jeshi la Polisi nchini Haiti, Leon Charles, kikundi hicho kinajumuisha raia 26 wa Colombia na Wamarekani wawili wenye asili ya Haiti.

Mpaka sasa, watuhumiwa 17 wameshakamatwa wakiwamo Wamarekani hao, huku wengine wanane wakiendelea kusakwa.

Washukiwa wengine kadhaa waliuawa kwa risasi katika mapambano na Polisi katika mji mkuu wa Port-au-Prince.

Mapema Jumatano, kundi kubwa la watu waliokuwa na silaha walivamia makazi binafsi ya rais na kuanza kushambulia.

Mke wa Rais Moise, Martine alijeruhiwa katika mashambulizi hayo na kukimbizwa Florida, Marekani kwa matibabu na inaelezwa anaendelea vizuri.

Haijafahamika mara moja nani aliyenyuma ya mipango ya mauaji ya kiongozi huyo na kwa lengo gani.

Ingawa Waziri mkuu wa mpito wa Haiti, Claude Joseph, ambaye anaongoza nchi hiyo kwa sasa aliiambia BBC kwamba, rais huyo mwenye umri wa miaka 53 alikuwa anakabiliana na aliowaita manguli wenye ushawishi mkubwa nchini humo.

**BBC**

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA CHETI



**ESTER JAMES POYO** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.1141/0012** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **SWILLA SEKONDARI** mwaka **2009.** Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DAR/OST/RB/327333/2021.**

116351702

## KUPOTEA KWA RESULT SLIP



**RYANN JOACKIM PERERA** anatangaza kupotelewa na Result slip ya kidato cha nne chenye index namba **S2549/0069** iliyotolewa na **ALPHA HIGH SCHOOL** mwaka **2020.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DAR/CHU/RB/331686/2021.**

116351802

## KUPOTEA KWA CHETI



**MEHBOOB R.J. JESSANI** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S0335-0150** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **AGA KHAN MZIZIMA SEKONDARI** mwaka 1984. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DSM/PHQ/RB/343741/2021.**

116352102

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**TAJINDERSINGH TZ BANSAL** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI YENYE NAMBA ZA USAJILI **T606 ABM.** YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI. TAARIFA YA POLISI: **DOD/DOD/RB/325257/2021.**

116351902

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**Mahakama ya Mwanzo MAKOLE**
**Wilaya ya DODOMA**
**MADAI NAMBARI 268/2020**

**MDAI.................. HILDA FILEMON KIRA**
**DHIDI YA**
**MDAIWA................ RAYMOND PIUS NYENZA**

**KWA: RAYMOND PIUS NYENZA**
**IRINGA MJINI**

Kwa kuwa Mdai ameleta madai yake kwamba **MADAI YA PESA TASLIMU TSH.1,200,000/=**

Kwa hiyo unahitajika kuhudhuria binafsi katika mahakama hii siku ya **JUMATATU** tarehe **12/07/2021** saa 2:30 asubuhi kwa kujibu madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ya kukatwa shauri hilo ni lazima kuleta mashahidi wako na hati zote zinazohusu shauri hilo kwa ajili ya kujiitetea katika shauri hilo.

Angalia kama hakuhudhiria siku ilitajwa hapo juu. Mahakama ikithibitisha kama umepokea kuitwa kuitwa shaurini hii itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa.

Hati hii imetolewa kwa amri yangu na chapa ya Mahakama hii leo tarehe **9/7/2021**

116352302

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**MAHAKAMA YA HAKIMU MKAZI MBEYA**
**SHAURI LA MADAI NAMBA. 41/2019**
**JOSEPH CHEVILE NA WENZAKE**
**7..............................WADAI**
**DHIDI YA**
**LUCOMOS COMPANY LTD...............WADAIWA**
**MAJALIWA MWAMAKULA**
**KWA :**
**MAJALIWA MWAMAKULA**
**WITO WA KUONESHA SABABU**

***(Amri ya21r,35(1)Sura ya 33iliyofanyiwa marekebisho mwaka 2019)***

Kwa kuwa Joseph Chevile na wenzake 7 wamefungua maombi ya kukaza hukumu kwa mfumo wa kukamata mali zenu.

Hivyo unatakiwa **KUFIKA** Mahakama ya Hakimu Mkazi Mbeya mnamo Tarehe 13/7/2021 saa 08;30 asubuhi bila kukosa ili uoneshe sababu kwanini ukazaji huo wa Hukumu usitekelezwe kama ilivyoombwa..

Hati hii imetolewa kwa Amri yangu pamoja na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 5/7 2021

**HAKIMU MKAZI**
**MAHAKAMA YA HAKIMU MKAZI**
**MBEYA**

116352502

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**BENEDICTO JOSEPH MBEYAA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **ISUZU FORWARD** yenye namba za usajili **T 585 BYX** Lenye chassis namba **FRR12LC3004535. KADI namba 8370055.** Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa polisi. Taarifa ya polisi RB. Namba **IRI/IRI/RB/339981/2021.**

116352602

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(MCA/84)**
**Mahakama yamwanzo ya KAWE**
**Wilaya ya KINONDONI**
**Madai nambari 22 ya 2021**
**Mdai MERINA CHARLES NJUGA**
**Amdai**
**Mdaiwa NIGANILE NELSON MWAKAJOKA**
**Kwa. NIGANILE NELSON MWAKAJOKA**
**KIZUDI**
**DAR ES SALAAM**
**Kwakuwa mdai/wadai ameleta/wameleta madai yao kwamba**
**FIKA MAHAKAMANI BILA KUKOSA KUJIBU MADAI YA PESA SIKU YA 06/8/2021**

Kwahiyo unahitajiwa/mnahitajiwa kuhudhuria binafsi katika mahakama hii siku ya IJUMAA tarehe 06/8/2021 saa 2:30 asubuhi kwa kujibu madai haya .nakwa kuwa siku hiyo ya kukatwa shauri hilo nime lazima kuleta mashahidi wake/wenu na hati zote zinazohusu shauri hilo kwaajili ya kujitetea katika shauri hilo.

Angalia kama hukuudhuria siku iliyotajwa hapo juu.mahakama ikithibitisha kama umepokea kuitwa shaurini hii,itaweza kuto ahukumu kuwa hati hii,itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa

Hati hii yatolewa kwa amri ysngu na chapa ya mahakama hii leo tarehe 08/7/2021.

116352602

**OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 0782253676**

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Tupigie

0782253676

Nipashe
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# HADITHI

TOM alipooa alidhani kuwa ataishi kwa amani, furaha na kupata utulivu kama inavyokuwa kwa rafiki na wenzake wote waliofanya hivyo.
Siku zote ndoa ni masikilizano, maelewano, na anayeoa hupata furaha na heshima. Kinyume chake, kwake imekuwa ni misukosuko, mikosi na balaa. Badala ya kuwa ndoa yenye furaha, akajiingiza kwenye mtego hatari ambao hata baada ya kuufahamu, hakuweza kuutegua tena. Alichelewa. Ukawa ni mwanzo ni vilio, maafa na mtiririko wa mambo ya kushangaza.
Hebu pata kila nakala ya gazeti hili kufuatilia kisa hiki cha kushangaza na kusikitisha.

# Namsaka mke wangu-2

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**

Pamoja na kwamba alipenda sana kuishi kwa dada yake Kigamboni Mikwambe na huko ndiko taratibu za posa na kila kitu zilifanyikia, lakini aliishi zaidi Morogoro maeneo ya Kichangani.

Licha ya kwamba nako alifanya nao mawasiliano na kuambiwa nako hajaonekana, lakini alitaka aende kama alivyofanya kwa ndugu wengine ili apate uhakika wa asilimia zote.

Ni yeye pekee ndiye aliyeonekana kutumia nguvu kubwa kumpata kuliko ndugu wa bi harusi. Alijua sababu yake. Ni kwamba wanajua hayupo sehemu hatarishi. Mtu anayeandika kuwa anaondoka ni kwamba anajua anakokwenda. Kama asingeandika chochote, hata ndugu wangeungana naye kumsaka Farida. Hata yeye alijua hajapotea. Hajakufa. Na wala hayupo kwenye sehemu hatari.

Anachojuliza tu ni kwamba "Yupo kwa nani? Kwa nini? Na kwa nini iwe hivyo wakati yeye tayari ni mke wa mtu?" Alijua mtu anayepotea na ndugu zake wanakuwa na wasiwasi sana ni yule ambaye anapotea ghafla na hakuna taarifa yoyote kuwa yupo wapi.

Kila kitu kilikuwa moyoni mwa Tom. Wasiwasi, hasira, wivu vilimchoma

"Nitakwenda Morogoro. Nitakwenda kusaka mke wangu." Alisema akizuidi kufuta machozi akiwa peke yake varandani kwenye sofa.

************************

Ni siku ya pili sasa Tom yupo Morogoro. Alifikia kwenye nyumba moja ya kulala wageni. Alikwenda hadi kwao maeneo ya Kichangani. Kwa sababu wazazi wake wote wawili walishafariki, aliwakuta baadhi ya ndugu zake. Uzuri ni kwamba wanamfahamu mume wa Farida. Alikaribishwa kwa heshima zote.

Tayari walishapata taarifa za kutoweka kwa ndugu yao Farida. Huko nako hadithi zikawa ni zilezile. "Hatujamuon." "Hajafika."

Kazi yake ikawa ni usiku kwenda alikofikia na kesho yake kwenda ukweni. Alishaanza kukata tamaa. Aliazimia kesho yake kurejea Dar es salaam.

Akiwa anatoka nyumbani kwa wakwe zake, kurudi alikofikia, Tom aliona kuna mtu anakuja nyuma yake kwa hatua za haraka haraka.




**"Kwanza wewe hujaniambia unamtafuta nani. Niambie, halafu nikishajua, ninachanganya na ya wale waliyokuwa wanasema ndiyo nitajua ni hilo linalolijua mimi au kuna lingine." Alisema mlevi yule na kabla hata Tom hajaongea lolote aliongeza.**

Akawa makini kuangalia nini kitatokea. "Bro bro, kwani wewe unamtafuta nani?" Aliulizwa tena bila salamu.

Alimtazama kijana huyo aliyeokana ni mlevi. Ni moja kati ya wale watu ambao yeye akiamka asubuhi anachowaza ni kunywa tu. Maisha yake ni kunywa pombe. Hakumbuki kula, kufua, au kitu chochote kile.

Nguo zake zilikuwa kuukuu na chafu. Nywele zake zilionyesha kuwa zilikuwa chui na paka na kitana.

Kidogo amtimue. Lakini alikumbuka msemo wa mama yake mzazi miaka mingi iliyopita kuwa asimdharau mtu yoyote. Hata anayeonekana dhalili mbele za watu.

"Kuna mtu namtafuta." Alijikuta akimjibu.

"Unajua bro, wewe hujui tu. Nilipita kwa masista zangu pale nikakukuta pale. Sasa wale ni jirani zangu. Waliokuwa wanaongea, ikanionyesha kuwa wewe kuna mtu unamtafuta hapa Morogoro sawa?" Aliuliza kwa sauti yake ya kilevi.

Pamoja na ulevi wake alionekana mwenye busara, kwani hakuwa anaongea kwa kupayuka.

"Walikuwa wanaongeaje?" Tom aliuliza haraka haraka.

"Subiri kwanza kaka. Usiwe na wasiwasi. Mambo mazuri hayataki haraka. Haya ambayo nitakwambia, nitayasema kwa hatua. Moja baada ya nyingine. Halafu mimi watu si wananiona sina akili, sijui mlevi, sasa nitakuonyesha kwa vitendo." Alisema huku akiwa anayumbayumba.

Sasa Tom alionekana kumhitaji zaidi mlevi yule kuliko yeye alivyokuwa anahitajika.

Mambo yaligeuka. Mwanzo ni kama jamaa yule mlevi ni kama alikuwa anajipendekeza. Labda ampige mzinga pesa ya kunywa. Lakini sasa Tom ambaye ilikuwa kidogo amtimue, sasa alianza kumbembeleza.

Ilionekana ni kama ana taarifa nyingi ambazo yeye hazifahamu. Ana vitu vingi ambavyo ninaweza kusababisha kupatikana kwa mkewe Farida.

"Enhee, hebu niambie walikuwa wanaongea nini? Na kuna nini?"

"Kwanza wewe hujaniambia unamtafuta nani. Niambie, halafu nikishajua, ninachanganya na ya wale waliyokuwa wanasema ndiyo nitajua ni hilo linalolijua mimi au kuna lingine." Alisema mlevi yule na kabla hata Tom hajaongea lolote aliongeza.

"Kwanza twende ukanipige na kinibu ili nipate nguvu ya kuongea na wewe vizuri."

Chochote ambacho alihitaji kilichokuwa ndani ya uwezo wake kwa wakati ule angeweza kukipata, ili mradi tu apate kujua mkewe yuko wapi. Tom alikubali. Na alimwambia kila kitu hadi alivyoroka na kuacha kimeseji ndani.

************************

"Sikiliza nikwambie, wale ndugu zake wanakuzuga tu. Mkeo huwa anakuja pale usiku, anakaa kidogo halafu anaondoka." Alisema mlevi yule alijitambulisha kwa jina la Gaga.

Alikuwa anaongea kama mzaha hivi, lakini maneno yale walimshtua sana Tom. Pamoja na kwamba yalimfanya kuamini kuwa mkewe yu hai, lakini hakutegemea kama anaweza kufanya jambo kama lile.

Amtoroke nyumbani. Arudi Morogoro ambako alizaliwa kusomea na kukulia. Halafu asiwe anaishi kwao, badala yake awe anakuja usiku na kuondoka.

"Anaishi wapi? Anaishi kwa nani? Na kwa nini anakuja usiku kwa ndugu zake na kurejea huko anakoishi?" Hayo ni baadhi ya maswali yaliyoanza kumiminika kichwani.

Gaga alinyanyua tena kinibu cha pombe kali na kuimimina kinywani, huku akiwa amefumba macho.

Aliweka kinibu chini, akapanua mdomo na kutoa sauti ya kuonyesha kuwa alichokuwa anakunywa ni pombe kali sana.

"Mama muuza, ongeza nyingine. Leo nimekuja na tajiri mkubwa sana." Aliagiza kwa mbwembwe.

Akarekebisha sauti yake na kuwa ya chini.

"Unasikia bwana. Mimi siwezi kujua anaishi wapi. Ila ninachojua ni kwamba huwa anamuona anakuja usiku, halafu halali, anaondoka. Kingine ni kwamba leo usiku kama una muda, twende kwa Msamvu kwenye baa moja ya Mwenda. Kuna wakati huwa anaonekana huko."

"Huwa anakuja na nani pale nyumbani?" Tom aliuliza.

"Peke yake. Sijawahi kumuona anakuja na mtu."

"Na hapo kwenye baa ya Mwenda anapoonekana, huwa yupo na nani?"

"Hapo sasa sijui, kwa sababu kuna mtu aliniambia tu kuwa yule Farida mbona anaonekana sana kwenye baa ya Mwenda wakati ameolewa Dar es salaam, wiki moja tu iliyopita?"

Tayari Tom alishajua kuwa mkewe yupo, na huwa anawasiliana na ndugu zake, japo ndugu hawataki kumwambia ukweli.

Kwa sababu haiwezekani ndugu wa Morogoro wawe wanamuona usiku anakuja kuwasalimia, halafu washindwe kuwaambia wenzao wa Dar kuwa ndugu yao yuko hai.

**ITAENDELEA JUMAMOSI**

## HABARI MICHEZO



# POGBA 'hajawahi kukaribia Juve'

**TURIN,** Italia

MKURUGENZI wa zamani wa michezo wa Juventus, Fabio Paratici amesema mabingwa hao wa Serie A kamwe hawajawahi kukaribia kumsajili tena nyota wa Manchester United, Paul Pogba.

Pogba anaingia kwenye mwaka wake wa mwisho pale United na nyota huyo wa Ufaransa majaliwa yake bado yamebakia kuwa na sintofahamu, huku ikielezwa anahusishwa na Juventus, Real Madrid na Paris Saint-Germain.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28, ambaye aliondoka United kwenda Juve mwaka 2012 kabla ya kurudi tena Old Trafford mwaka 2016, kwa muda mrefu amekuwa akihusishwa na Bianconeri hao, lakini Paratici ametupilia mbali uvumi huo.

"Paul Pogba kurudi Juventus? Nafikiri ni ngumu sana," amesema Paratici, ambaye kwa sasa ni Mkurugenzi wa soka pale Tottenham, akiiambia Sky Sport.

"Kamwe hakujakuwa na muda ambao tulikaribia kumsajili na kumrudisha tena Juventus."

Pogba na Ufaransa walitolewa kwenye michuano ya Euro 2020 katika hatua ya 16 na Uswisi kwa mikwaju ya penalti baada ya muda wa kawaida na ule wa zaidi kumalizika kwa sare.

# PSG, CITY ZAMGOMBEA MESSI



**PARIS,** Ufaransa

KLABU za Paris Saint-Germain na Manchester City zote zinafuatilia kwa makini hali ya usajili wa Lionel Messi baada ya mchezaji huyo sasa kuwa huru, kwa mujibu wa ukurasa wa kwanza kwa gazeti la Mundo Deportivo.

Awali iliripotiwa kwamba, Barcelona wamefikia makubaliano ya kumwongezea mkataba mpya nyota huyo wa Argentina mara baada ya kumaliza mkataba wake mwezi uliopita.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 34 mwaka jana alitangaza kutaka kuondoka pale Barcelona, lakini baadaye akaamua kubakia klabuni hapo.

Mkataba wa Messi pale Barcelona ulimalizika Juni 30, mwaka huu lakini inaonyesha anaweza asisaini tena kwa miamba hao wa LaLiga, ambao kwa sasa wapo kwenye matatizo ya kifedha.

Na sasa Mundo Deportivo limeripoti kuwa Messi bado hajafikia makubaliano na Barca na hivyo miamba wa Ligi Kuu Ufaransa, Ligue 1, PSG na wale wa Ligi Kuu England, Manchester City zinamtolea macho.

Mshindi huyo mara sita wa tuzo ya Ballon d'Or kwa sasa yupo na Timu ya Taifa ya Argentina kwenye michuano ya Copa America.

## Camavinga njia nyeupe kusajiliwa na United

**MANCHESTER,** England

KLABU ya Manchester United imefungua mazungumzo rasmi na mawakala wa kiungo wa Rennes, Eduardo Camavinga kwa ajili ya kumsajili mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 18.

Baada ya kumsajili Jadon Sancho, United wanafanya kazi kusajili beki wa kati mpya na pia kiungo mpya msimu huu wa joto.

Camavinga anaangaliwa sana na Bodi ya Manchester United kama mmoja wa malengo ya muda mrefu ya klabu hiyo.

Klabu ya Paris Saint-Germain pia imekuwa ikimfuatilia kwa muda mrefu kutaka kumsajili mchezaji huyo.

United wameanza mawasiliano ya moja kwa moja na Camavinga na Rennes wako tayari kujadili juu ya ada ya euro milioni 30 kwani wanaweza kumpoteza mchezaji huyo bure katika kipindi cha majira ya joto.

Camavinga atamaliza mkataba wake Juni, 2022 na mchezaji huyo hana haraka kuamua muskabadhi wake huku United na PSG wakiwa kipaumbele kumsajili mchezaji huyo.



# Giroud akaribia kutua Milan

**MILAN,** Italia

KLABU ya Chelsea inakaribia kukubali dau lenye thamani ya pauni milioni 1.7 ili kumuuza Olivier Giroud kwa AC Milan ya nchini Italia.


Kwa mujibu wa Sky Sport Italia, mchezaji huyo wa kimataifa wa Ufaransa mwenye umri wa miaka 36 yuko mbioni kusafiri kwenda Italia kwenye vipimo vya afya kabla ya kusaini na Milan kwa dau la euro milioni mbili.

Miamba hao wa Ligi Kuu Italia, Serie A, wanatakiwa kulipa ada ya awali ya paundi 860,000 pamoja na paundi nyingine 860,000 kwa nyongeza kulingana na uwezo wa mchezaji na kufuzu kwa klabu kwenye hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu ujao.

Giroud alisaini mkataba mpya wa mwaka mmoja huko Chelsea msimu uliopita wa joto na mwezi uliopita klabu ilimwongezea miezi 12 zaidi.

Arsenal ilimuuza Giroud kwenda Chelsea kwa pauni milioni 18 mnamo Januari 2018, miaka sita baada ya kumsajili kutoka timu iliyoshinda taji la Ligue 1 Montpellier kwa pauni milioni 10.8.

Giroud amefunga mabao 39 katika mechi 119 pale Stamford Bridge, akishinda mataji matatu makubwa, pamoja na taji la Ligi ya Mabingwa mnamo mwezi Mei, mwaka huu.





# RONALDO sasa kubaki Juventus

**TURIN,** Italia

CRISTIANO Ronaldo nyota wa kikosi cha Juventus atasalia ndani ya kikosi hicho licha ya kuelezwa kwamba Real Madrid na Manchester United wanahitaji saini yake.

Msimu uliopita nyota huyo ilibakia kidogo aondoke kwa sababu alikuwa anatajwa kuelekea Manchester United ambao walikuwa wanatajwa kuiwinda saini yake.

Wakala wa mchezaji huyo Jorge Mendes inaelezwa ameomba nyota huyo aongezewe mkataba ndani ya kikosi hicho cha Juventus.

Mkataba wake ndani ya Juventus umebakiza mwaka mmoja kwa kuwa alisaini dili la miaka mitatu akitokea Real Madrid na Mei, mwaka huu ilikuwa inaelezwa alikuwa anafanya mazungumzo na Kocha Mkuu wa Manchester United, Ole Gunnar Solksjaer ili amrudishe ndani ya Old Trafford.

Msimu uliopita raia huyo wa Ureno alifunga jumla ya mabao 36 katika mechi 44 ambazo alicheza ndani ya Juventus.

# Fati rasmi kuanza mazoezi Barca

**BARCELONA,** Hispania

ANSU Fati ataweza kuanza mazoezi ya mapema ya msimu na Barcelona ifikapo Julai 12, mwaka huu kama wachezaji wenzake wengine.

Kinda huyo anaendelea kupona vizuri kutokana na jeraha lake la goti ambalo lilimfanya kuwa nje ya dimba kwa muda mrefu na kwa idhini ya madaktari wa klabu, atafanya mazoezi kutoka mwanzoni mwa msimu wa mapema.

Baada ya operesheni nne, Fati anajisikia vizuri tena na sasa anatarajia kurudisha kiwango chake ambacho kilimfanya aanze katika kikosi cha kwanza cha Barcelona na kikosi cha Timu ya Taifa ya Hispania.


Lakini, Fati hatatumika haraka kwenye mechi za maandalizi, kwani klabu itahitaji kuwa makini zaidi kuhusu afya yake kwa mujibu wa Marca.

"Kwanza, hatafanya mazoezi pamoja na wachezaji wenzake tangu mwanzo. Fati atafanya mazoezi peke yake mpaka atakaporudi kwa kasi nzuri," ilisema taarifa ya Barcelona kwenda kwa waandishi wa habari.

"Halafu matumaini ni kwamba ataweza kucheza mechi kadhaa za kirafiki kwa nia ya kuwa kwenye kikosi cha mchezo wa kwanza wa LaLiga wa msimu dhidi ya Real Sociedad Agosti 15."



# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# LIVERPOOL YAJIWEKA PAZURI KWA MBAPPE

### ●●● Ni baada ya mshambuliaji huyo kushikilia uamuzi wake wa kukataa kusaini mkataba mpya...

**LIVERPOO,** England

KLABU ya Liverpool inayoshiriki Ligi Kuu England inaongoza kwenye mbio za kuwania kumsajili mshambuliaji nyota wa Paris Saint-Germain, Kylian Mbappe, kwa mujibu wa RMC.

Majaliwa ya Mbappe pale kwenye jiji la Paris yametawala vichwa vya vyombo vya habari katika siku za hivi karibuni.

Mbappe amekuwa akitajwa kuwaniwa na Real Madrid kwa muda mrefu, baada ya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22 kuweka wazi kwamba hana mpango wa kuongeza mkataba pale PSG.

Mkataba wa Mbappe na PSG unamalizika mwishoni mwa msimu wa 2021-22 na amekuwa akihusishwa sana kujiunga na miamba wa La Liga, Real Madrid.

PSG bado hawajafanikiwa kumshawishi Mbappe kusaini mkataba mpya na nyota huyo wiki iliyopita alinukuliwa akisema hana mpango wa kufanya hivyo, kwa sababu anataka kuondoka na kwenda kutafuta changamoto mpya.

Na sasa kwa mujibu wa ripoti ya RMC ya jana Ijumaa, Liverpool ndio wanaongoza katika mbio za kuwania saini ya kumsajili mchezaji huyo wa kimataifa wa Ufaransa ambaye alikosa penalti dhidi ya Uswisi na timu yake kutolewa kwenye michuano ya Euro 2020 katika hatua ya 16.

Ripoti hiyo imebainisha kuwa, Liverpool wanajiandaa kutuma ofa rasmi kwa PSG kwa ajili ya kumsajili kipindi cha dirisha kubwa la majira ya joto.

## KWA UFUPI

### PSG YATUA KWA MESSI

KLABU ya Paris St-Germain imetoa ofa ya mkataba kwa fowadi wa Argentina, Lionel Messi mwenye umri wa miaka 34, ambaye kwa sasa ni mchezaji huru baada ya kumaliza mkataba wake na Barcelona. Hata hivyo, miamba hao wa LaLiga bado wana matumaini ya kumpa mkataba mpya mshindi huyo mara sita wa Ballon d'Or. (***AS***)

### DE BEEK NJIA MOJA

MANCHESTER United ipo tayari kumwachia Donny van de Beek kuondoka klabuni hapo huku kukiwa na taarifa kwamba anawaniwa na Real Madrid, ambao wanamtaka kiungo huyo wa Uholanzi mwenye umri wa miaka 24 kwa mkopo. (***Star***)

### NIGUEZ ATAJWA LIVERPOOL

LIVERPOOL inafikiria kumsajili kiungo wa Atletico Madrid, Saul Niguez mwenye umri wa miaka 26. (***La Razon***)

### SANCHES ANUKIA EPL

LIVERPOOL pia inawaniwa kumsajili kiungo wa Lille na Ureno, Renato Sanches mwenye umri wa miaka 23, lakini wanakabiliwa na ushindani kutoka kwa Arsenal ambao nao wanamtaka nyota huyo wa zamani wa Bayern Munich. (***Onze Mondial***)

### ARSENAL YAJIPANGA GOLINI

ARSENAL wapo tayari kufikiria kumsajili golikipa wa West Brom na England, Sam Johnstone mwenye umri wa miaka 28, kama dili la kumpata nyota wa Sheffield United, Aaron Ramsdale (23), litashindikana. (***Star***)

### ALLEGRI AMTAKA POGBA

KOCHA wa Juventus, Massimiliano Allegri ameitaarifu klabu juu ya mpango wake wa kutaka kumsajili, Paul Pogba (28), kutoka Manchester United. Kiungo huyo ambaye anatarajiwa kumaliza mkataba wake na Old Trafford ifikapo mwaka 2022, alishinda taji la Serie A akiwa na Juve wakati wa kipindi cha kwanza cha Allegri klabuni hapo. (***90 Min***)

### SPURS YAMGEUKIA VLAHOVIC

KLABU ya Tottenham Hotspur inampango wa kumsajili straika wa Fiorentina, Dusan Vlahovic mwenye umri wa miaka 21. (***Corriere dello Sport via Sport Witness)***

### SPURS KUMSAJILI COADY

KLABU ya Tottenham Hostpur inatarajiwa kushindana na Everton katika jaribio la kumsaijili beki wa England, Conor Coady kutoka Wolves. (***Football Insider***)

### GUENDOUZI HUYO LILLE

KIUNGO wa Arsenal, Matteo Guendouzi mwenye umri wa miaka 22, anakaribia kukamilisha usajili wa kutua Marseille. (***Goal***)

### SOCIEDAD MAMBO MAGUMU

REAL Sociedad imeshindwa katika jaribio lake la kumsajili mlinzi wa kushoto wa Benfica, Nuno Tavares mwenye umri wa miaka 21, ambaye anawaniwa pia na Arsenal. (***Mail***)

### JAKONOVIC KITAELEWEKA

KOCHA wa Sheffield United, Slavisa Jokanovic amesema atajaribu kumsajili kiungo wa Norway mwenye umri wa miaka 23, Sander Berge, ambaye anahusishwa na Arsenal. ***(Mirror)***

HABARI MICHEZO

# Zanzibar yajipanga CECAFA Wanawake

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

MABINGWA wa Ligi Kuu ya Wanawake Zanzibar, New Generation Queens wamesema wamejipanga kufanya vizuri katika mashindano ya kusaka tiketi ya kushiriki Fainali za Klabu Bingwa Afrika (CECAFA) yanayotarajiwa kufanyika kuanzia Julai 17, mwaka huu nchini Kenya.

New generation iko katika Kundi B pamoja na timu ya Benki ya Biashara ya Ethiopia na Yel Joint Stars kutoka Sudani Kusini.

Meneja wa New Generation Queens, Farid Mohammed, alisema timu hiyo inaendelea vyema programu zake za mazoezi ili kuhakikisha wachezaji wake wanaimarika na kwenda kuiwakilisha vizuri Zanzibar katika michuano hiyo itakayochezwa kwa mara ya kwanza.

"Ratiba tumeiyona na kocha anaendelea na mpangilio wake wa mazoezi huku tukiendelea kuzifuatilia kwa karibu timu pinzani ikiwamo kupata video zao ili kuwafahamu kabla ya kukutana nao katika mechi za michuano hii," alisema Farid.

Kiongozi huyo pia aliipongeza Wizara ya Michezo Zanzibar kwa misaada mbalimbali waliyotoa kwa timu hiyo ambayo imesaidia kupunguza changamoto walizokuwa nazo katika maandalizi.

Pia amewaomba wadau wa soka wa Zanzibar kuupa kipaumbele mpira wa miguu wa wanawake kama ilivyo katika michezo mingine ambayo wanawake wanashiriki ili wapate mafanikio.

# Nyota chipukizi tenisi uwanjani

**Na Shufaa Lyimo**

MASHINDANO ya tenisi ya vijana wenye umri wa miaka 12 hadi 20 yanatarajiwa kufanyika leo kwenye viwanja vya Gymkhana jijini Dar es Salaam.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Kocha Mkuu wa Klabu ya Gymkhana, Salum Mvita alisema leo la kuandaa mashindano hayo ni kuinua vipaji vipya vya wachezaji wanaochipukia.

Mvita alisema wanaamini kupitia michuano hiyo watapata nyota wapya watakaojiunga katika klabu mbalimbali za mchezo huo ambazo zinahitaji kujiendeleza na kujiimarisha kuelekea kwenye mashindano mbalimbali yatakayofanyika hapo baadaye.

"Wikiendi hii tutakuwa na mashindano ya vijana ambayo huwa tunapenda kuyafanya kwa sababu wanafunzi hawaendi shuleni, tunaomba wazazi wawalete watoto wao kushiriki michuano hiyo," alisema Mvita.

Kocha huyo aliongeza kwa kuwakumbusha wazazi na walezi kuwapa ruhusa vijana wao ya kushiriki michezo badala ya kukaa nyumbani kwa sababu michezo ni afya na mazoezi yanasaidia kujenga mwili.

"Pia tunaiomba serikali itusaidie kuboreshea viwanja vya michezo, tunawakumbusha vijana wenyewe kuthamini michezo kwa sababu imesaidia kutoa fursa ya kwenda nje ya nchi kujiendeleza," Mvita alisema.

# SIMBA QUEENS YAPANIA KUFANYA KWELI KIMATAIFA

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Simba Queens, Mussa Hassan 'Mgosi' amesema wamejipanga kupeperusha vyema bendera ya Tanzania katika mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika kwa Wanawake yanayotarajiwa kufanyika kuanzia Julai 17, mwaka huu nchini Kenya.

Katika mashindano hayo ya kusaka wawakilishi wa Ukanda wa Afrika Mashariki na Kati (CECAFA), Simba Queens imepangwa Kundi A ikiwa pamoja na Lady Doves WFC Uganda na PVP FC kutoka Burundi.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, Mgosi alisema ameona ratiba hiyo ya makundi na kuongeza hakuna timu ngumu au mbaya kwa sababu klabu zote ni mabingwa wa nchi wanazotoka.

Mgosi alisema alianza maandalizi ya michuano hiyo mapema kwa sababu wanahitaji kushiriki katika fainali zitakazofanyika baadaye nchini Misri na watakwenda Kenya kushindana.

Kiungo huyo wa zamani wa Simba na Timu ya Taifa ya Tanzania (Taifa Stars), alisema wamejiandaa kuipa heshima klabu yao kwa kufuata nyayo za kaka zao, Simba ambayo msimu huu ilifanya vizuri zaidi katika michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

"Tumekuwa tukifatilia timu zote, kwa bahati nzuri timu tulizopangwa nazo tumekuwa tukizifatilia kwa ukaribu ikiwamo Lady Dove WFC ambao jana (juzi) walicheza mechi yao ya mwisho na kutangaza ubingwa wa ligi ya Uganda,".

"Kwa Burundi ambayo inawakilishwa na PVP FC ni watu wetu wa karibu kwa sababu wachezaji wetu wawili, Joele Bukuru na Asha Djafar wametoka katika timu hiyo hivyo wanaifahamu vizuri na tutaweza kuwatumia nyota wetu hao kupata taarifa zao," alisema Mgosi.

Aliongeza kulingana na maandalizi waliyofanya, anaamini watakwenda Kenya kupambana katika kila mechi kufanya ili wafikie malengo yao ya kuwa mmoja ya timu ambayo itakayoshiriki kwenye fainali hizo za kwanza za michuano hiyo.

Mgosi alisema baada ya kuona kundi lao, leo (jana) wamekutana na uongozi wa klabu hiyo kwa ajili ya kupanga taratibu za safari ikiwezekana timu hiyo kwenda Kenya mapema au kuweka kambi mkoa wa karibu ambao hali ya hewa ya baridi kulingana na nchini wanayokwenda kushiriki michuano hiyo.

Kundi B katika mashindano hayo inaundwa na timu ya Benki ya Biashara ya Ethiopia, Yel Joint Stars (Sudan Kusini) na New Generation Queens ya Zanzibar huku Scandinavia WFC (Rwanda), FAD (Djibout) na Vitiga Queens ya Kenya zikiwa kwenye Kundi C.

Kila kundi litatoa timu moja itakayofuzu kushiriki katika fainali hizo za kwanza za Ligi ya Mabingwa ya Wanawake Afrika.



Kiongozi wa bendi ya muziki wa dansi ya Stara Thomas, mwimbaji Stara Thomas (wa pili kushoto), akitoa burudani katika Maonyesho ya Kimataifa ya Biashara Dar es Salaam kwenye viwanja vya Mwalimu Nyerere maarufu Sabasaba jijini jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Namungo haina haraka na usajili

**Na Adam Fungamwango**

MABOSI wa Namungo FC wamesema hawana haraka ya kufanya usajili sasa hivi kwa sababu wanasubiri Ligi Kuu Tanzania Bara imalizike na hatimaye kupokea ripoti kutoka kwa Kocha wao, Hemed Suleiman 'Morocco'.

Mwenyekiti wa klabu hiyo, Hassan Zidadu, aliliambia gazeti hili jana mpaka sasa hawajasajili mchezaji yoyote na wala hawatasajili mpaka watakapopokea mapendekezo ya kocha wao na si vinginevyo.

Hata hivyo amesema klabu yake itasajili mchezaji yeyote atakayetakiwa hata kama anatoka katika timu kubwa hapa nchini ikiwamo Simba.

"Hatuwezi kusema chochote kwa sasa, hatujapata ripoti ya mwalimu. Tunasubiri ripoti yake baada ya msimu kumalizika atatukabidhi, sasa kama ni mabadiliko makubwa au madogo, yatategemea na kocha amesema nini," alisema mwenyekiti huyo.

Zidadu alisema kama ilivyo kwa timu nyingine, Namungo FC inahitaji marekebisho na kuingiza baadhi ya wachezaji kwenye kikosi hicho ili kuwa imara zaidi.

"Mabadiliko yatafanyika. Hata Simba ambayo inasemekana iko vizuri bado tunasikia inasajili. Azam nao, Yanga nayo nasikia inasafiri huku na kule kusaka wachezaji, kwa hiyo usajili utakuwepo wakati ukifika," Zidadu alisema.

Kuhusu vita ya kugombea nafasi ya nne, mwenyekiti huyo alisema bado ni ngumu kwa sababu wanashindana na Biashara United ambayo iko juu yao.

Michezo

Jumamosi Julai 10, 2021

Nipashe



## Liverpool yajiweka pazuri kwa Mbappe

HABARI UK. 23



Mshambuliaji wa Yanga, Yacouba Sogne (kushoto), akijiandaa kumtoka beki wa Simba, Joash Onyango, katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyochezwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam Jumamosi iliyopita. Yanga ilishinda bao 1-0. **PICHA: MTANDAO**

# SIMBA, YANGA 'MOTO' KUWAKA

## ●●● Makocha watamba kushusha silaha kali msimu ujao ili kufanya vyema katika...

**Na Saada Akida**

WAKATI mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba, wakiendelea kujivunia uwekezaji wa mfanyabiashara, Mohammed Dewji 'Mo' kwa kujiandaa kufanya usajili imara zaidi, Kocha Mkuu wa Yanga, Nasreddine Nabi naye ametamba atanasa saini za nyota wapya sita ambao watakibadilisha kikosi chake.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa Simba, Didier Gomes, ameahidi timu yake itafanya mambo mazuri zaidi katika msimu ujao kwa kuhakikisha inasajili wachezaji wapya ambao wataifanya timu hiyo kuwa bora na tofauti ukilinganisha na misimu mingine iliyopita.

Gomes alisema timu yake bado inahitaji kuimarika zaidi na katika kuhakikisha hilo linafikiwa, anajiandaa kukutana na Ofisa Mtendaji Mkuu wa Simba, Barbara Gonzalez na Mo kwa ajili ya kufanikisha mapendekezo yake yanatekelezwa.

Kocha huyo alisema anafurahi kupata sapoti kutoka kwa viongozi hao wa juu ambao wamesaidia kikosi chake kuwa na wakati mzuri licha ya ushindani na changamoto mbalimbali wanazokutana nazo.

"Simba bado inaendelea kukua sana, nafurahi kuona Barbara na Mo Dewji wamekuwa wakinipa sapoti sana, nilikuwa na kikao nao kimoja jana (juzi), tulizungumza mengi ikiwamo usajili, lakini naamini msimu ujao utakuwa bora kwangu tofauti na makocha wengine walionitangulia," alisema Gomes.

Alisema alijiunga na timu tayari dirisha la usajili limeshapita lakini sasa yuko mwenyewe na tayari mapendekezo yake yameanza kufanyiwa kazi ikiwamo usajili kwa ajili ya kuimarisha timu hiyo kuelekea mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika msimu ujao.

Aliongeza tayari ana uhakika mkubwa wa kuteteta ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara na kazi iliyoko mbele yake ni kuimarisha kikosi chao kuelekea katika michuano ya kimataifa ambapo malengo yake ni kuona Simba inacheza hatua ya nusu fainali.

Kuhusu mechi tatu zilizobakia za ligi, Gomes alisema wamejipanga vizuri kuhakikisha wanaupa heshima ubingwa wao kwa kutopoteza mchezo hata mmoja.

Naye Nabi aliliambia gazeti hili ameutaka uongozi wa klabu hiyo kufanya maboresho ya usajili kwa kuwanasa wachezaji wapya wasiozidi sita ili kuhakikisha wanatengeneza kikosi bora kitakachoshindana kutwaa mataji katika msimu ujao wa mwaka 2021/22.

Ofisa Habari wa Yanga, Hassan Bumbuli alisema Nabi anafurahishwa na ubora wa kikosi walichonacho na ili kuwa imara zaidi ameelekeza kusajili wa wachezaji wapya ambao watakiongezea nguvu kuelekea msimu mpya ambao watashiriki mashindano ya kimataifa.

Bumbuli alisema udhamini mpya walioupata kutoka Azam Media utachochea klabu yao kupata mafanikio zaidi na kumaliza ukame wa kutwaa taji la Ligi Kuu Tanzania Bara ambazo watani zao wanalishikilia kwa misimu mitatu mfululizo.

"Tutajipanga kuhakikisha heshima ya Yanga inarejea, tutaimarisha kikosi chetu kama ambavyo kocha wetu atakavyopendekeza, tunajua kiu ya mashabiki wetu, tunataka kurejea kwenye ushindani," Bumbuli alisema.

Tayari Yanga imeshamalizana na beki wa kulia Mkongomani Shabani Djuma huku nyota wengine wanaotajwa ni pamoja na Lazarus Kambole, Marcey Vumbi Ngimbi, Dickson Ambundo, Bryson Raphael, na Denis Kibu, Abubeker Nassir, Anthony Akumu na Heritier Makambo.

# TFF yahofu kifungo FIFA

**Na Kulwa Mzee**

MAHAKAMA Kuu ya Tanzania inatarajia kutoa uamuzi wa ama kusimamisha au kutosimamisha mchakato wa uchaguzi wa Rais wa Shirikisho la Soka Nchini (TFF) ifikapo Julai 16, mwaka huu.

Uamuzi huo wa mahakama hiyo ulifikiwa jana mbele ya Jaji Edwin Kakolaki baada ya kusikiliza hoja ya mlalamikaji, akitaka uchaguzi uliopangwa kufanyika Agosti 7, mwaka huu usimamishwe huku walalamikiwa wakiomba maombi yatupwe kwa kuwa yakikubaliwa, TFF itafungiwa na Shirikisho la Soka la Kimataifa (FIFA).

Mlalamikaji katika shauri hilo ni Ally Salehe na mlalakiwa ni Bodi ya Wadhamini ya TFF, TFF na Mwenyekiti Kamati ya Uchaguzi.

Akimwakilisha mlalamikaji, Wakili Jeremiah Mtobesya alidai mteja wake aliondolewa katika mchakato kwenye hatua ya mahojiano wakati alitakiwa kuhojiwa kisha taarifa zake kuwekwa katika ubao wa matangazo ili endapo kuna anayepinga, awasilishe hoja zake. Alidai pingamizi likiwapo kunakuwa na usikilizwaji ndipo mgombea anaondolewa lakini hatua hizo hazikufanyika kwa mlalamikaji.

Wakili Mtobesya anadai utaratibu umekiukwa na madhara yake hayawezi kufidiwa na endapo amri hiyo haitatolewa mlalamikaji atapata hasara kwa kuwa ndiye anayeweza kupoteza zaidi kuliko TFF.

Akijibu, Wakili wa Walalamikiwa, Alex Muchunguzi, alidai kwamba katika kiapo cha mlalamikaji, hakuna hoja za msingi za kuifanya mahakama ifikie uamuzi wa kutoa zuio la muda la uchaguzi hadi kesi ya msingi namba 98 itakaposikilizwa.

Anadai hakuna mahali popote katika hati ya kiapo ambapo mlalamikaji aliandika malalamiko ya kukiukwa kwa utaratibu na kutokuwapo kwa taarifa zake katika ubao wa matangazo.

Wakili Muchunguzi alidai utaratibu upo, mlalamikaji alitakiwa kukata rufani katika Kamati ya Rufani ya Uchaguzi na kwamba masuala yanayohusu fedha yanashughulikiwa na Kamati ya Fedha.

Alidai kutolewa kwa zuio kutamwathiri zaidi mlalamikiwa namba mbili TFF, ikiwa ni pamoja na kufungiwa na FIFA kushiriki katika mashindano ya mpira wa miguu.

9 770856 541002 >

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042